

**HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU
(MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
FEDHA KWA MWAKA 2018/2019**

A: UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2017/18 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2018/19. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Kawaida pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2018/19.

2. Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara kwa nchi yetu na maelekezo yake ambayo

yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha huduma za Afya na Maendeleo ya jamii nchini.

Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kutoa msukumo mkubwa katika uanzishwaji wa viwanda vya kutengeneza Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi hapa nchini. Msukumo huo utaboresha huduma za afya kwa watanzania kama nyenzo muhimu ili kufikia Uchumi wa Kati.

3. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za afya kwa Watanzania hasa katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu, Afya ya Mama na Mtoto, magonjwa yasiyo ya kuambukiza pamoja na Afya ya Vijana. Wizara yangu itaendelea kutumia ushauri, nasaha, ushawishi na uzoefu wake ili kuhakikisha watanzania wanaweza kujikinga na maradhi na kujenga jamii ya Watanzania wenye Afya Bora.

4. Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaosaidia kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako tukufu

ambayo imetoa dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka 2018/19.

5. Mheshimiwa Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yako kwa weledi katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb)** katika utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

6. Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru **Mheshimiwa Selemani Jaffo (Mb)** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wake ulioniwezesha kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya ngazi ya msingi. Pia, ninawashukuru Mawaziri wa Wizara nyingine zote ambazo ushirikiano wao na Wizara yangu umechangia katika utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii.

7. Mheshimiwa Spika, kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Peter Serukamba (Mb)**, na Makamu Mwenyekiti, **Mheshimiwa Juma Nkamia (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyotoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa

ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya na maendeleo ya jamii nchini. Ninawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge.

8. Mheshimiwa Spika, ninatoa pole kwa watazania wote, waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga. Aidha, ninatoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Tanzania ya Viwanda.

9. Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2017/18, Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2018/19 pamoja na maombi ya fedha ambazo zitaiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake.

**B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MPANGO WA
MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

10. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Sera, Mipango Mikakati pamoja na makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini. Maeneo haya ya vipaumbele yameainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati 2016/17 – 2020/21, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2015-2020, na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's 2030). Aidha, Wizara imezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Sera ya Afya (2007) na Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2015 – 2020); Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Wazee (2003); na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (1979); na Mkataba wa Haki za Mtoto (1989)

11. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka wa fedha 2017/18, kupitia **Fungu 52**, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za serikali, Wakala wa Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za Afya katika maeneo yafuatayo;

a) Kuimarisha Huduma za Kinga, Tiba, na kuongeza usawa katika kutoa huduma za afya,

b) Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto ili kupunguza

- vifo vya wanawake wajawazito na watoto,
- c) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo katika vituo vya kutolea huduma za afya,
 - d) Kuimarisha miundombinu kwenye vyo vya mafunzo ya afya kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu,
 - e) Kuimarisha matibabu ya kibingwa nchini kwa kuendeleza ujenzi, upanuzi, ukarabati wa miundombinu na kufunga mitambo ya kisasa ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Benjamini Mkapa - Dodoma, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto; pia Hospitali za Rufaa za Kanda; Kanda ya ziwa (Bugando), Kanda ya Kaskazini (KCMC), Hospitali ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Kanda ya Kusini (Mtwara),
 - f) Kuimarisha mazingira ya ubia na ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi (PPP) katika utoaji wa huduma za afya,
 - g) Kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo vya kutolea Huduma za Afya,
 - h) Uimarishaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha huduma za afya.
 - i) Kuhamasisha wananchi kujiunga na Mifuko ya Bima za Afya kwa lengo la kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma za afya zenye uhakika.

12. Mheshimiwa Spika, kupitia **Fungu 53,** Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ilipanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- a) Kuratibu utekelezaji na ufuatiliaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22, kwa kutoa elimu kwa jamii na watoa huduma kwa waathirika wa ukatili kwa wanawake na watoto, uimarishaji wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto; Kuendeleza kampeni ya kukomesha ndoa za utotoni na mimba za utotoni katika mikoa yenye kiwango kikubwa cha ukatili ya Katavi, Shinyanga, Mara, Dodoma, Singida, Simiyu na Geita;
- b) kuimarisha upatikanaji wa haki, maendeleo na ustawi watoto ikiwemo kwa watoto walio katika mkinzano wa Sheria;
- c) Kuwezesha wazee wasiojiweza na watoto walio katika mazingira hatarishi kupata huduma za msingi;
- d) Kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo kwa kuzingatia rasilimali walizonazo;
- e) kuelimisha jamii hususan wanawake na katika ngazi ya Halmashauri kujiunga na VICOBA na SACCOS kwa ajili ya kuwawesha kiuchumi;
- f) Kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii katika makazi ya wazee, Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini, mahabusu za watoto na Shule ya Maadilisho; na
- g) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika vyuo na Taasisi za maendeleo na ustawi wa jamii.

Mapato na Matumizi ya Fedha – Fungu 52

13. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia **Fungu 52** (Afya), hukusanya mapato yake kupitia huduma za tiba zitolewazo na hospitali zilizo chini yake, tozo za huduma katika Taasisi mbalimbali, Bodi na Mabaraza, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi wa vitabu vya maombi ya zabuni, pamoja na makusanyo yatokanayo na utoaji wa huduma katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, Wizara pamoja na Taasisi zake imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi **162,891,572,942** sawa na **asilimia 72** ya lengo la mwakala kukusanya kiasi cha Shilingi **227,041,160,573** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato. Mafanikio haya yametokana na utaratibu wa kulipia huduma kupitia benki, uhamasishaji kuhusu kulipa maduhuli ya serikali, udhibiti wa makusanyo, kuongezeka kwa ari ya utendaji kazi, uboreshwaji wa huduma za Bima na Kuimarishwa kwa mfumo wa malipo kwa njia ya Ki-elektroniki.

14. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kupokea na kutumia jumla ya **Shilingi 1,077,701,892,000**. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi 291,895,940,000** sawa na **asilimia 27** ya bajeti yote ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na shilingi ni **Shilingi 785, 805, 952,000** sawa na **asilimia 72.9** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo .

15. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia Machi 2018, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 617,507,623,167** sawa na **asilimia 57** ya bajeti iliyoidhinishwa ya **Shilingi 1,077,701,892,000** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2018 ni **Shilingi 216,736,325,825,824 sawa na asilimia 74** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 68,814,900,939** zilitumika katika Matumizi Mengineyo (OC) ikiwa ni sawa na **asilimia 73.3** ya kiasi kilichotengwa na **shilingi 147,921,424,885** zilitumika kulipia mishahara (Fungu 52) sawa na **asilimia 65** ya kiasi cha fedha kilichotengwa. Aidha, Wizara imepokea kiasi cha shilingi 22,500,000,000 kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni na matibabu nje ya nchi.

Kwa upande wa **Miradi ya Maendeleo**, hadi kufikia Machi, 2018 kiasi cha **Shilingi 400,771,297,343** kilipokelewa, sawa na **asilimia 51** ya fedha zilizoidhinishwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 79,756,079,206** ni fedha za ndani sawa **asilimia 24** ya fedha iliyoidhinishwa. Fedha za nje zilizopokelewa ni **Shilingi 321,015,218,137.12** sawa na **asilimia 71** ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 82,515,009,463.82** na kuzipeleka **OR-TAMISEMI** kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma za dharura ikiwa ni pamoja na upasuaji wa akina akinamama wajawazito (CEmONC) ili kumtoa mtoto tumboni

pindi wanapokabiliwa na uzazi pingamizi. Kati ya fedha hizo **Shilingi 63,015,009,462.82** ni kutoka Benki ya Dunia na **shilingi 19,500,000,000.00** kutoka Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund).

Mapato na Matumizi - Fungu 53

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Fungu 53 (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto), ilitarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 2,101,874,000** kutokana na ada za wanafunzi kutoka katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli; uuzaji nyaraka za zabuni na ada mbalimbali za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 jumla ya **Shilingi 1,775,466,155** sawa na **asilimia 84** zilikusanywa.

17. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara kupitia Fungu 53 ilitengewa jumla ya **Shilingi 37,909,880,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 19,142,252,240** ni bajeti ya Mishahara, **Shilingi 16,161,349,760** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 2,606,278,000** ni kwa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018, jumla ya **Shilingi 18,352,527,400** sawa na **asilimia 48** zilipokelewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,848,331,727** sawa na asilimia **55** ni Matumizi Mengineyo; **Shilingi 8,470,927,127** sawa na **asilimia 44** ni Mishahara ya Idara pamoja na Taasisi zilizo chini

ya Wizara; na **Shilingi 1,033,268,546** sawa na **asilimia 40** fedha za Miradi ya Maendeleo.

18. Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 ulikuwa kama ifuatavyo:

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU CHINI YA IDARA KUU YA AFYA

HUDUMA ZA KINGA

Chanjo

19. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Mwaka 2017/2018, Wizara iliratibu ununuzi wa chanjo Rota; dozi **2,383,700** kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kuhara kwa watoto; PCV 13 dozi **1,000,000** kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Nimeria; chanjo za Surua Rubella dozi **3,326,200** kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Surua na Rubella; BoPV zilinunuliwa dozi **3,966,000** kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio), pentavalenti dozi **1,179,000** kwa ajili ya kukinga Donda Koo, Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini, na Mafua ya Influenza dozi **2,000,000** kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa Pepo Punda, BCG dozi **2,000** za kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu na dozi **999,600** kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa ulemavu wa ghafla.

Vile vile Wizara ilisimamia shughuli za utoaji wa chanjo kwa watoto ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa kitaifa na kimataifa yanafikiwa. Takwimu za Januari hadi Desemba 2017 zinaonyesha kuwa **asilimia 101.2** ya Watoto waliolengwa nchini walipatiwa chanjo zote muhimu ili kuwakinga na magonjwa. **Mnamo mwezi Desemba 2017, Serikali ya Tanzania ilipongezwa kwa kufikia kiwango cha juu cha chanjo kwa asilimia 97 ya uchanjaji watoto kwa chanjo ya pentavalent kwa takwimu za mwaka 2016.** Lengo la Mkakati wa Dunia kupitia Shirika la Afya Duniani ni nchi kufikia kiwango cha uchanjaji wa **asilimia 90.** Shirika la Afya Duniani na wadau wameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kufikia kiwango hicho ambapo inakuwa nchi ya Tatu barani Afrika ikitanguliwa na **Zambia** yenye kiwango cha **asilimia 99** ikifuatiwa na **Rwanda** yenye **asilimia 98.** Taarifa ya Wataalam wa Chanjo ulimwenguni (GNAP Assessment Report 2017) ilibainisha kwamba wastani wa kiwango cha uchanjaji barani Afrika ni **asilimia 74** na kiwango cha uchanjaji cha Dunia ni **asilimia 86.** Kwa hali hiyo Tanzania ni moja ya nchi iliyopata mafanikio makubwa katika eneo hili kwa kufikia kiwango kilicho juu ya wastani wa bara la Afrika na cha Dunia.

20. Mheshimiwa Spika, saratani ya mlango wa kizazi ndio inayoongoza nchini kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa na pia kusababisha vifo vya wanawake wengi. Kwa mujibu wa takwimu za Taasisi ya Saratani Ocean Road za mwaka 2017/18, **asilimia 32.8** ya wagonjwa wa saratani nchini ni wa saratani ya mlango wa kizazi ikifuatiwa na saratani ya matiti yenye **asilimia 12.9.** Saratani nyingine ni *Kaposi Sarcoma* (11.9%), saratani ya koo (10.9%),

saratani ya kichwa na shingo (7.5%), saratani ya matezi (5.4%), saratani ya damu (4.7%), saratani ya kibofu cha mkojo (3.0%), saratani ya ngozi (2.6%) na saratani ya tezi dume (2.1%).

21. Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, saratani ya mlango wa kizazi inazuilika kwa kuwapatia chanjo wasichana kuanzia miaka 9 hadi 14. Katika kukabiliana na saratani hiyo, mwaka 2017/18 Serikali imeanza kutoa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi (HPV Vaccine). Kutokana na upatikanaji wa dozi kutoka kwa wazalishaji, kwa mwaka 2018 chanjo hiyo imeanza kutolewa kwa wasichana wenye miaka 14, ambapo, hadi Desemba 2018, Wizara imelenga kuwafikia wasichana **616,734** wa umri huo. Chanjo hiyo ni salama na inatumika katika nchi mbalimbali za Afrika ikiwemo **Rwanda, Uganda, Afrika ya Kusini, Zambia** na **Lesotho**. Kupitia Bunge lako Tukufu, nawasihi wazazi na walezi wenye watoto kuhakikisha binti zetu wanapata chanjo hiyo muhimu ili kuwakinga dhini ya saratani ya mlango wa kizazi.

Afya na Usafi wa Mazingira

22. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira inayotekelezwa katika Halmashauri zote nchini. Kupitia Kampeni hii idadi ya kaya zenye vyoo bora imeongezeka kutoka **1,996,413** Juni 2017 hadi **2,414,094** Desemba, 2017. Katika kipindi hicho, kaya zenye sehemu maalum za kunawa mikono zimeongezeka kutoka **611,257** hadi **1,056,604**. Kwa upande wa Vituo vya Tiba, jumla ya Vituo **277** vilijenga au kukarabati vyoo kwa kiwango cha ubora unaotakiwa. Aidha, Wizara iliendesha Mashindano ya Taifa ya Usafi wa Mazingira katika Halmashauri 184 ambapo Washindi

wa kwanza, wa pili, na watatu walizawadiwa kama ifuatavyo: **Kundi la Majiji na Manispaa** washindi ni Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, jiji la Arusha na Manispaa ya Iringa; **Halmashauri za Miji**, washindi ni; Mji wa Njombe, Kahama na Tunduma; na upande wa Halmashauri za Wilaya washindi ni **Halmashauri ya Wilaya** ya Meru, Njombe na Makete ambapo pia vijiji vya Kanikele-Njombe DC, Nambala-Meru DC na Lyalalo-Njombe DC viliibuka washindi. Katika Kundi la Hospitali, washindi ni Arusha Lutheran Medical Center, St. Francis Hospital-Ifakara na Mt. Meru Hospital ya Arusha. Kwa kundi la Hoteli za Kitalii washindi watatu wa juu ni Hyatt Regency Dar es Salaam, Kilimanjaro Hotel, Mount Meru Hotel na Adden Palace Hotel-Mwanza. **Wizara ilitoa zawadi ya gari jipya aina ya NISSAN kwa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Treкта la kubeba taka kwa Halmashauri ya Mji wa Njombe na zawadi ya Pikipiki kwa Halmashauri na Vijiji vilivyoibuka washindi.** Nitumie fursa hii kuzipongeza Halmashauri zilizofanya vizuri na kuzitaka Halmashauri nyingine kuongeza jitihada katika utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii ya 2009 kupitia kada ya Maafisa Afya ngazi ya Kata hadi Tarafa.

23. Mheshimiwa Spika, Katika kudhibiti magonjwa ya mlipuko hususani Kipindupindu, Wizara kwa kushirikiana na wadau pamoja na vyombo vya habari imetekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na; kuandaa mpango wa miaka 3 (2018-2020) wa kudhibiti Ugonjwa wa Kipindupindu nchini, sambamba na kufuatilia hali ya ugonjwa wa kipindupindu nchi nzima. Wizara

yangu ilituma timu za wataalam za kukabiliana na ugonjwa huo (Rapid Response Teams) katika mikoa ya Kigoma, Tanga, Iringa, Mbeya, Dar es Salaam, Ruvuma na Songwe ili kudhibiti ugonjwa wa Kipindupindu. Wizara ilitoa matamko 9 kwa jamii kupitia Vyombo vya Habari 13 (Luninga, Radio na mikutano ya waandishi wa habari) kuhusu hali ya ugonjwa wa kipindupindu nchini na mikakati ya kuudhibiti.

24. Mheshimiwa Spika, Wizara imesambaza vidonge vya kutakasa maji (aqua tabs) **milioni 6.72**, na pia jumla ya tani 50 za *chlorine granules* zimesambazwa katika Mamlaka za Maji katika Mikoa 19 ambayo ni Kigoma, Katavi, Mwanza, Rukwa, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Arusha, Mara, Singida, Tanga, Geita, Simiyu na Pwani ili kutibu vyanzo vya maji. Aidha maji katika *Water bowzers* 64 katika miji ya Dar es Salaam na Morogoro yametibiwa kwa kutumia *jumbo aqua tabs* makasha 132 ya vidonge 6 kila moja. Mafunzo yametolewa kwa wauza maji ya magari wapatao 213 katika mikoa ya Mwanza, Mara, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Pia jumla ya visima virefu (Boreholes) 18 vimechimbwa katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mara na Mwanza. Wizara imesambaza jumla ya pakiti za *Oral Rehydration Salt (ORS)* **milioni 7.36** pamoja na dawa na vifaa tiba kwa ajili ya kudhibiti kipindupindu katika Mikoa 9 ya Dar es Salaam, Pwani, Manyara, Arusha, Geita, Mara, Morogoro, Dodoma na Mwanza.

25. Mheshimiwa Spika, Hali ya ugonjwa wa Kipindupindu nchini inaendelea kudhibitiwa. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi

2018 jumla ya wagonjwa wa kipindupindu 4,508 na vifo 92 viliripotiwa katika Mikoa ya Songwe, Dodoma, Ruvuma na Mbeya. Nitoe rai kwa viongozi katika mikoa yote nchini kulifanya suala la kupambana na ugonjwa wa kipindupindu kuwa ni agenda ya kudumu katika vipaumbele vyao.

26. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kutoa huduma ya chanjo ya homa ya manjano katika vituo 20 vikiwemo vituo vya Afya Bandari, Mipakani, Viwanja vya Ndege na Mnazi Mmoja kwa wasafiri wanaokwenda kwenye nchi zenye maambukizi ya ugonjwa huo. Jumla ya dozi **14,000** za chanjo na vyeti **22,000** viliagizwa na kusambazwa kwenye vituo vya afya mipakani Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Mwalimu Julius Nyerere, Bandari ya Dar es Salaam, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro, Uwanja wa Ndege Songwe, Tunduma, Kasumulu, Mtambaswala, Rusumo, Namanga, Uwanja wa Ndege Mwanza, Kigoma, Mtukula, Tarakea, Holili, Horohoro, Bandari ya Tanga, Bandari Kavu Isaka, Sirari na Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

27. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto nchini, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka 5 wa mwaka 2016 hadi 2020 unaolenga kuboresha afya ya uzazi, mama, watoto na vijana pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 292 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2020. Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imezingatia maeneo makuu matatu ambayo ni: **huduma ya uzazi wa mpango, huduma wakati wa ujauzito na huduma wakati wa kujifungua.** Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa

huduma bora, inayofikiwa kwa wanawake wote, kabla ya ujauzito, wakati wa ujauzito, na wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua, kama muhimili muhimu wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto chini ya miaka mitano.

28. Mheshimiwa Spika, huduma za uzazi wa mpango ni muhimu katika kuimarisha afya ya mama na mtoto pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara imenunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango katika vituo vya huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na: Depo-provera vichupa **2,986,853**; dawa ya kidonge yenye kichocheo kimoja (Microval) mizunguko **19,357**; Vipandikizi **227,976**; Vitanzi **61,599**; dawa ya dharura (emergency contraceptives) **28,953**; Vipandikizi vya Jadelle **209,050**; Microgynon mizunguko **1,500,000**; Kondomu za Kiume **6,902,646**; na kondomu za kike **61,599**. Aidha jumla ya **wateja 519,817** walifikiwa na huduma ya uzazi wa Mpango kupitia utaratibu wa mkoba (out reach services) na **424,595** walipata huduma kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya.

29. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya afya wakati wa ujauzito ni afua muhimu katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kwani matatizo mengi yanaweza kuzuilika, kugundulika na kutibiwa kama wanawake wajawazito watahudhuria kliniki ya wajawazito na kupimwa na wahudumu wenye ujuzi ndani ya **wiki 12 tangu wanapokuwa wamejigundua kuwa wanaujauzito**. Katika kipindi cha Julai 2017/18, Wizara iliendelea kuhakikisha kwamba huduma kwa wanawake wajawazito zinapatikana sambamba na kuelimisha wajawazito kuhudhuria kliniki. Kulingana na TDHS 2015/16, asilimia 51 ya wanawake wajawazito

walihudhuria angalau mara 4 ikiwa ni kiwango cha chini cha mahudhurio kinachotakiwa. Aidha, kulingana na taarifa kutoka vituo vya kutolea huduma ya afya, hadi kufikia mwezi Februari 2018 asilimia 81.7 walihudhuria angalau mara moja. Lengo ni kufikisha asilimia 70 ya wanawake wajawazito kuhudhuria kliniki angalau mara 4 katika kipindi cha ujauzito ifikapo mwaka 2020. **Nitumie fursa hii kuwahimiza wajawazito wote kuhudhuria kliniki kama inavyoshauriwa.**

30. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa **huduma bora wakati wa kujifungua** ikiwemo huduma ya dharura wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua, ni muhimu sana ili kuepuka vifo vitokanavyo na uzazi. Huduma kwa matatizo haya hupatikana tu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na kutolewa na watoa huduma wenye ujuzi. Katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhamasisha na kuhimiza wanawake wajawazito kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma. Mwelekeo ni kwamba Idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma inaendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia **68.5 mwezi Februari 2018 katoka asilimia 64 mwaka 2015/16.** Napenda kutoa wito kwa wanawake wajawazito wote nchini, wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya ili kupunguza vifo na changamoto za uzazi kwa mama na mtoto.

31. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za afya ya Uzazi na Watoto, dawa za sindano aina ya Oxytocin (kwa ajili ya kuzuia

mama mjamzito kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua) vichupa **1,141,208** na Magnesium Sulphate (dawa ya kuzuia kifafa cha mimba) vichupa **76,219**; Fefol (dawa ya kuongeza wingi wa damu) vidonge **55,888,500**; Vidonge vya Amoxicillin myeyuko **4,086,946** na Zinc/ORS **1,084,780** (dawa ya kuzuia kuharisha) vilinunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya katika Halmashauri mbalimbali nchini. Hatua hii imeokoa maisha ya wanawake wajawazito ambao walipata matatizo ya kutokwa na damu nyingi au kifafa cha mimba wakati na baada ya kujifungua. Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuhakikisha fedha za uzazi salama zinapatikana kwa wakati.

32. Mheshimiwa Spika, kupunguza **vifo vya watoto chini ya miaka mitano** ni moja ya kipaumbele cha Wizara. Kulingana na **Mpango Mkakati wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa 2016-2020**, Serikali imedhamiria kuwa ifikapo 2020 vifo vya watoto wa chini ya mwezi mmoja vipungue kutoka 21 hadi 16 katika kila vizazi hai 1,000; vifo vya watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja kutoka 45 hadi 25 katika kila vizazi hai 1,000 na vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano kutoka 54 hadi 40 katika kila vizazi hai. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018. Wizara iliwajengea uwezo watoa huduma ya afya Katika kuwahudumia watoto wagonjwa kwa njia jumuishi (Integrated Management Child Illness-IMCI). Mafunzo haya yalitolewa kwa watoa huduma **1,342** katika mikoa ya Mwanza, Geita na Mara. Aidha watoa huduma 296 kutoka katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Rukwa na Katavi walijengewa uwezo jinsi ya kutoa huduma ya dharura kwa mtoto mgonjwa sana.

33. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi ya Vituo vya Afya ili viweze kutoa huduma za dharura za upasuaji ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kutoa mtoto tumboni (CEmONC) pindi mama mjamzito anapohitajika. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inaboresha vituo vya afya takribani 208 (kama ilivyoainishwa katika hotuba ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI) ili kuviwezesha kutoa huduma za CEmONC. Hadi Machi 2018, maboresho ya vituo hivyo yalikuwa yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Maboresho haya yanahusu ujenzi wa vyumba vya upasuaji (Theatres), wodi ya wakinamama wajawazito (Martenity/Labour wards), vyumba vya maabara na nyumba za watumishi. Kukamilika kwa maboresho haya kutaongeza idadi ya vituo vinavyomilikiwa na Serikali vyenye uwezo wa kutoa huduma hiyo ya CEmONC kufikia 283 kati ya Vituo vya Afya 527. Hii itakuwa sawa na asilimia 53.7 ya vituo vya afya vya umma vitakavyoweza kutoa huduma za upasuaji wa dharura kutoka asilimia 21 mwezi Juni 2016.

34. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeandaa mpango wa **mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi** wa sekta ya afya ili kuboresha huduma za Upasuaji wa Dharura. Jumla ya watumishi 200 kutoka katika Halmashauri 96 wanatarajiwa kujiunga na mafunzo ya mwaka mmoja ya utoaji wa dawa ya usingizi (Anaesthesia) mwezi Mei, 2018. Aidha, Wizara yangu imejiwekea mkakati maalumu wa kuboresha huduma kwenye vituo vilivyokarabatiwa kwa kutekeleza yafuatayo: Kutoa kipaumbele cha ajira hususani katika vituo vyenye

uhaba mkubwa, kutawanya watumishi kutoka kwenye maeneo yenye watumishi wengi kuhamishiwa kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa pamoja na kuandaa program maalumu ya wataalamu (madaktari bingwa) kutembelea vituo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora na salama za upasuaji kwa wajawazito.

Wizara imeendelea kushirikiana na Wadau katika kutoa **Elimu ya Uzazi Salama** kwa jamii kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo Runinga, Redio na ujumbe kwa njia ya simu. Takriban jumla ya wajawazito **952,484** wamefikwa kwa kutumia ujumbe kwa njia ya simu kuwahamasisha kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kuwaelimisha umuhimu wa kuhudhuria kliniki katika kipindi chote cha ujauzito na baada ya kujifungua hadi mtoto anapotimiza miaka mitano. Lengo ni kufikia wajawazito **1,800,000** kwa mwaka.

35. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti saratani za via vya uzazi (Reproductive cancers) ikiwemo saratani ya mlango wa kizazi, saratani ya matiti na saratani ya Tezidume. Aidha, katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kupima na matibabu ya Mabadiliko ya awali ya Saratani ya Mlango wa kizazi na saratani ya matiti ambazo ndizo zinazoongoza nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanzisha **vituo vipya 100 vya uchunguzi na tiba ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi** katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, Songwe, Geita, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Tanga, Lindi, Mtwara, Simiyu, Mara na Ruvuma. Vilevile, Wizara ilinunua na kusambaza

mashine 100 za cryotherapy, 9 za LEEP na mitungi 173 kwa ajili ya matibabu ya dalili za awali za Saratani ya mlango wa kizazi. Pia, watoa huduma 186 kutoka mikoa iliyotajwa hapo juu, walipata mafunzo ya uchunguzi na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi, na madaktari 18 walipatiwa mafunzo ya namna ya kutoa matibabu kwa kutumia mashine za LEEP.

36. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanzisha kampeni ya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na saratani ya matiti, ambapo kila kituo kinachotoa huduma kimeagizwa kutenga siku maalum kila mwezi kwa ajili ya kuwafanyia wanawake uchunguzi wa saratani hizo pamoja na utoaji huduma za matibabu katika halmashauri zote nchini. Kila kituo (Hospitali na Kituo cha Afya) kimepangiwa lengo maalum ili kuwezesha kufikiwa kwa wanawake **3,000,000**, ifikapo mwezi Desemba 2018.

Udhibiti wa UKIMWI

37. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Desemba 2017, jumla ya watu wapatao **5,164,297** walipimwa VVU na kupewa majibu ya hali zao za afya, ambapo watu **145,104** (sawa na asilimia **2.8**) kati yao waligundulika kuwa na maambukizi na kuanzishiwa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI. Aidha, takwimu za hadi Desemba, 2017 zinaonesha kuwa jumla ya watu wanaoishi na VVU wapatao **965,081** walikuwa wanatumia dawa za kufubaza VVU, ikiwa ni sawa na **asilimia 69** ya watu **1,400,000** wanaokadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI nchini na kati yao watoto walikuwa **55,304** ambao ni sawa na **asilimia 5.7**. Kutokana na takwimu hizo Tanzania

tumebakiza **asilimia 21** kufikia lengo la dunia la **asilimia 90** ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kuanzishiwa dawa za kufubaza VVU ifikapo mwaka 2020. Wizara imeweka mikakati mbalimbali ili kufikia lengo hilo.

38. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilifunga mashine mpya 5 zenye uwezo mkubwa wa kupima sampuli nyingi kwa siku na kubainisha wingi wa virusi vya UKIMWI (HIV Viral Load) na utambuzi wa maambukizi kwa watoto waliozaliwa na wakina mama wanaoishi na VVU (HIV Early Infant Diagnosis). Mashine tatu (3) zimefungwa katika Maabara ya Hospitali ya Temeke, Mashine moja imefungwa katika maabara ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na moja imefungwa katika Maabara ya hospitali ya Bugando, Mwanza.

39. Mheshimiwa Spika, Huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT), zimeendelea kutolewa, ambapo, jumla ya akina mama wajawazito **1,967,260** sawa na asilimia **98.7%** ya akina mama **1,993,639** walipatiwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU. Kati yao akina mama **79,242** sawa na asilimia 4 waligundulika kuwa wanaishi na VVU. Akina mama **79,240** sawa na asilimia **99.9** ya akina mama wenye maambukizi ya VVU walipatiwa dawa (ARV) kwa ajili ya kufubaza virusi vya UKIMWI. Aidha jumla ya Watoto **72,960** sawa na asilimia **92** walipata kipimo cha awali cha utambuzi wa maambukizi ya VVU ambapo watoto **2,918** sawa na asilimia **4** walikutwa na

maambukizi. Kiwango hicho cha maambukizi kinaashiria kuendelea kupungua kwa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, na hivyo kuiwezesha nchi kufikia malengo ya Kimataifa ya kutokomeza kabisa maambukizi ya VVU kwa watoto. Hivi sasa, maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ni **asilimia 4.9** kutoka asilimia **12 mwaka 2011**.

Huduma za Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma

40. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na mkakati wake wa Udhibiti wa ugonjwa wa Kifua Kikuu na Ukoma ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi 2017, Serikali ilinunua na kusambaza dawa za Kifua Kikuu na Ukoma. Katika kuhakikisha Serikali inaboresha matibabu ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa watoto, mwezi Machi 2018, Wizara yangu ilizindua matumizi ya **dawa mpya za kifua kikuu kwa watoto**. Dawa hizi mpya ni za mseto (RHZ/RH) ulioboreshwa, zina ladha nzuri ya matunda, zinayeyuka kwa urahisi zikiwekwa kwenye maji na hivyo hazihitaji kukatwakatwa ili kupata dozi sahihi.

41. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeongeza wigo wa upatikanaji wa **huduma za ugunduzi wa ugonjwa wa kifua kikuu kwa kutumia vipimo vya vinasaba (genexpert)** katika wilaya zote nchini ili kuongeza kazi ya kuwagundua wagonjwa wengi wa TB na kuwatibu. Kwa mwaka 2017/18, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ilinunua na kusambaza mashine za "genexpert"

189 ikilinganishwa na mashine 66 zilizokuwepo mwaka 2015. Vilevile, Wizara imepokea jumla ya vitendanishi (Catridges) boksi 3,675 ambazo zitatumika katika ugunduzi wa ugonjwa wa kifua kikuu kwa kutumia vipimo vya vinasaba (gene-xpert). **Teknolojia ya mashine hizi inatuwezesha kupata majibu ndani ya masaa 2 badala ya kusubiri kwa zaidi ya masaa 24** kama ilivyo kwa njia za kawaida za hadubini (Microscopes). Aidha, mashine hizi zina uwezo wa kupima usugu wa dawa za kifua kikuu wakati huo huo wa upimaji wa makohozi, na hivyo kugundua kifua kikuu sugu kwa urahisi zaidi. Mashine hizi zimesambazwa kwenye hospitali zote za rufaa za kanda, mikoa, wilaya na baadhi ya vituo vikubwa vya afya.

42.Mheshimiwa Spika, Katika kudhihirisha nia ya serikali ya kushirikiana na Sekta binafsi katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu hasa kuongeza idadi ya wagonjwa wa TB wanaogunduliwa kutoka **asilimia 40** hadi **asilimia 70** mwaka 2020, Wizara yangu imekabidhi mashine za gene-xpert tano (5) kwa hospitali binafsi za jijini Dar es Salaam. Hospitali zilizopokea mashine hizi ni Aga Khan, Hubert Kairuki, Regency Medical Center, TMJ na Hindul Mandal. Mashine hizo kila moja ina thamani ya **Shilingi milioni 38**. Tumeanza na hospitali hizi zenye viwango vikubwa vya wagonjwa wanaohudumiwa na pia kwa kuzingatia utayari wa hospitali hizi katika kutoa huduma za kifua kikuu sanjari na malengo ya Serikali yetu ya awamu ya tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa jamhuri ya

Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi wote. Kadhalika, ushirikishwaji huu wa Sekta Binafsi katika kutambua wagonjwa wa kifua kikuu umeonesha **ongezeko la wagonjwa wa TB wanaoibuliwa na sekta binafsi kutoka wagonjwa 3,476 mnamo mwaka 2014 hadi wagonjwa 7,281 katika mwaka 2017 ambao ni sawa na 10.4%** waligunduliwa na sekta binafsi. Nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sekta binafsi kwa ushiriki wao katika kutokomeza TB nchini.

43. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuongeza wigo wa **huduma za matibabu ya wagonjwa wa kifua kikuu sugu nchini.** Katika kipindi cha mwaka 2017 hadi Machi 2018 Wizara iliongeza vituo 41 na kufanya jumla ya vitu vinavyotoa huduma hiyo kufikia vituo 63 ikilingalishwa na kituo kimoja cha hospitali Maalum ya Kibong'oto mwaka 2015. Mafanikio haya yamewawezesha wagonjwa wa kifua kikuu sugu kutibiwa katika hospitali za karibu wakitokea majumbani kwao badala ya kutegemea Hospitali Maalum ya Kibong'oto, ambako pia walikuwa wanakaa kwa muda mrefu. Mikoa yenye vituo hivyo vilivyoweza kuanzisha matibabu ya wagonjwa chini ya ugatuzi ni Dar es salaam, Kagera, Geita, Mtwara, Lindi, Mbeya, Pwani, Morogoro, Tanga, Unguja, Tabora, Kigoma, Mwanza, Arusha, Rukwa na Simiyu. Vile vile, Wizara imeanzisha matibabu ya muda mfupi **kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu kufupisha tiba hiyo kutoka miezi ishirini ya hapo awali mpaka miezi tisa kwa wagonjwa wanoakidhi vigezo.**

44. Mheshimiwa Spika, Katika kushughulikia madhara yatokanayo na Kifua Kikuu cha mapafu (Pulmonary TB) pamoja na magonjwa mengine sugu ya mapafu (Chronic Lung Diseases), Wizara yangu imezindua kituo cha kisasa cha huduma za afya mahala pa kazi yaani *Occupational Health Services Centre* kwenye hospitali maalum ya Kibong'oto.

45. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **ugonjwa wa Ukoma,** Wizara ilifanya uchunguzi wa vimelea vya Ukoma katika ngazi ya jamii kwenye Wilaya 6 zenye maambukizi makubwa katika mikoa ya Geita (Chato), Lindi (Liwale), Mtwara (Nanyumbu), Morogoro (Kilombero) na Tanga (Mkinga na Muheza). Katika zoezi hilo takriban watu **500** wamefanyiwa uchunguzi, ambapo watu **54** sawa na asilimia **10.8** waligundulika kuwa na vimelea vya ugonjwa wa ukoma na kuanzishiwa matibabu, takriban watu **300** wamepatiwa tiba kinga.

Udhibiti wa Malaria

46. Mheshimiwa Spika, Malaria imeendelea kuwa sababu ya vifo vya wananchi wengi ambapo kwa takwimu za Januari – Desemba 2017, jumla ya wagonjwa **5,592,844** wameugua ugonjwa huu, kati yao wagonjwa **4,421** walifariki kutokana na ugonjwa wa Malaria. Katika kuendeleza juhudi za kupunguza maambukizi ya malaria nchini; Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za udhibiti wa malaria. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi, 2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau imenunua **Dawa mseto (Alu)** jumla ya **dozi 12,916,050,** vitepe vya **mRDT 21,428,725,**

vidonge vya SP dozi 6,899,700 kwa ajili ya tiba-kinga kwa wajawazito na dawa ya sindano ya **Artesunate vichupa 1,668,464** kwa ajili ya matibabu ya malaria kali na kusambazwa katika vituo vya huduma za afya kupitia Bohari ya Dawa nchini (MSD). Ili kuendelea kuwakinga wananchi dhidi ya malaria, na hasa kulenga makundi maalum; wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja, Serikali imesambaza jumla ya **vyandarua 4,726,763** kwa jamii bila malipo kupitia wanafunzi shuleni na kupitia kliniki za wajawazito na watoto (Chandarua Kliniki).

47. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, kuhusu Afua ya kuangamiza viluwiluwi vya mbu katika mazalia (larviciding), Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeratibu zoezi la usambazaji wa viuadudu vya **kibailojia (biolarviciding)** jumla ya **lita 236,420** katika Halmashauri zote nchini, na Halmashauri zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa afua katika maeneo yao. Kutokana na juhudi kubwa za Serikali kwa kushirikiana na wadau wake, katika kutekeleza mikakati ya udhibiti iliyopendekezwa na WHO, kiwango cha maambukizi ya malaria kimepungua kwa takriban **asilimia 50** kutoka **asilimia 14.8** mwaka 2016 hadi **asilimia 7.3** mwaka 2017. Katika kutambua juhudi hizi kubwa na kipaumbele cha Serikali yetu katika kudhibiti malaria, **Shirika la Afya Duniani limetoa tuzo kwa Wizara yangu kwa kuthamini mchango wa Serikali yetu na mafanikio yaliyopatikana katika kudhibiti malaria nchini.**

Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele

48. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau, imeendelea na juhudi za kudhibiti na kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele (matende, mabusha, usubi, kichocho, minyoo ya tumbo na trachoma) kwa njia ya kingatiba kupitia ugawaji wa dawa kwenye jamii zenye kiwango kikubwa cha maambukizi katika Halmashauri zote 185 za hapa nchini. Aidha, hadi kufikia Machi 2018 Serikali imetoa **dozi takribani 52,537,325** kwa watu wapatao **24,373,159**. Kati yao, watu **12,669,612** walipatiwa Kingatiba ya magonjwa wa Matende na Mabusha, watu **4,894,307** walipewa kingatiba ya Ugonjwa wa Usubi, watu **6,917,303** walipewa kingatiba ya Kichocho, watu **22,041,327** walipewa kingatiba ya Minyoo ya Tumbo, na watu wapatao **3,536,764** walipewa kingatiba dhidi ya ugonjwa wa trachoma.

49. Mheshimiwa Spika, Katika kupunguza madhara yatokanayo na magonjwa haya, Wizara kwa kushirikiana na Wadau ilitoa huduma ya upasuaji wa mabusha kwa wagonjwa wapatao **1,639** kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Lindi. Pia, takribani wagonjwa **6,535** walipatiwa huduma ya kurekebishiwa kope katika mikoa ya Tanga, Ruvuma, Arusha, Manyara, Mtwara, Lindi, Pwani na Dodoma.

50. Mheshimiwa Spika, Kutokana na utekelezaji wa afua mbalimbali za kudhibiti magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, jumla ya **Halmashauri 93 zimefanikiwa kupunguza kiwango cha maambukizi** ya ugonjwa wa matende na mabusha na **hivyo kuondolewa kwenye orodha ya Halmashauri zenye**

maambukizi makubwa zinazoshiriki katika zoezi la Kingatiba kulingana na vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO). **Kiambatisho Na. 1** kinaainisha Halmashauri zilizofanikiwa kupunguza Maambukizi Makubwa ya ugonjwa wa Matende na Mabusha. Haya ni mafanikio makubwa kwani Watanzania wapatao **20,446,532** wanaoishi katika halmashauri hizi hawapo tena katika hatari ya maambukizi ya magonjwa haya.

Huduma za Lishe

51. Mheshimiwa Spika, Katika kupambana na utapiamlo nchini, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Lishe imetoa matone ya nyongeza ya vitamin A kwa watoto wa kati ya miezi sita na miaka mitano sambamba na dawa za minyoo kwa watoto wa umri kati ya mwaka mmoja na miaka mitano. Matone hayo ya vitamini A hutolewa kwa awamu mbili yaani mwezi Juni 2017 na Desemba 2017. Jumla ya watoto **7,824,360** sawa na asilimia **93** walipatiwa matone ya vitamini A kwa mwezi Juni, 2017 na watoto **6,837,920** sawa na asilimia **92** walipatiwa dawa za minyoo. Kwa mwezi Desemba 2017, jumla ya watoto **8,007,114** sawa na asilimia **93** walipatiwa matone ya vitamini A na watoto **6,977,047** sawa na asilimia **92** walipatiwa dawa za minyoo.

52. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na asasi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali inaendelea kutoa virutubishi muhimu vya madini na vitamini kwa ukuaji wa mwili na akili kupitia urutubishaji wa unga wa ngano, unga wa mahindi na mafuta ya alizeti. Jumla ya mikoa 16 yenye Halmashauri 59 imefikiwa kupitia urutubishaji wa unga wa ngano, unga wa mahindi

na mafuta ya alizeti sawa na asilimia 31. Aidha, asilimia 82 ya kaya zote nchini zinatumia chumvi iliyoongezwa madini joto na hivyo kuziepusha dhidi ya ugonjwa wa Goita. Vile vile, mikoa inayotekeleza urutubishaji wa chakula kwa kutumia virutubishi nyongeza kwenye chakula cha kawaida kwa watoto wenye umri wa miezi 6 hadi 59 katika ngazi ya jamii (Home Food Fortification) imeongezeka na kufikia 16.

53. *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu imendelea kutoa huduma za matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto, kupitia uboreshaji wa Hospitali kwa kuzijengea miundombinu kwenye wodi za kulaza watoto, kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa chakula dawa na vifaa vya kupimia hali ya Lishe pamoja na kujengea uwezo wa watoa huduma. Aidha, Hospitali zinazotoa matibabu ya utapiamlo mkali zimeongezeka na kufikia 32. Lengo la Serikali ni kuhakikisha Hospitali zote za Mikoa na Wilaya zinatoa huduma za matibabu ya utapiamlo mkali.

Elimu ya Afya kwa Umma

54. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza afya zao dhidi ya magonjwa, kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara na kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya. Katika kutoa elimu hiyo, Wizara ilitayarisha na kusambaza vipeperushi, majarida, mabango na Makala mbalimbali zilizokuwa na ujumbe wa kuelimisha jamii kuhusu magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza. Elimu hiyo ilitolewa maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Shuleni, makundi ya vijana, vijijini, mijini kwa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kama vile radio na Televisheni, pamoja na mitandao ya kijamii kama *Twitter*,

WhatsApp na face book. Wizara kupitia mpango wa Elimu ya Afya kwa Umma imeandaa mkakati wa mawasiliano utakaowezesha namna ya kuwasiliana kwa haraka wakati wa majanga na milipuko ya magonjwa, tayari timu za mikoa ya mipakani zimeelimishwa juu ya mkakati huo. Aidha, Wizara imekamilisha **ujenzi wa studio ya radio na televisheni** ambavyo vimeanza kurekodi vipindi vitakavyorushwa nchi nzima kwa ajili ya kuelimisha jamii ya Watanzania kuhusu masuala mbalimbali ya afya.

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza Nchini

Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa miongozo ya udhibiti wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa kitaifa wa usafishaji figo (Dialysis) na Mwongozo wa mafunzo ya huduma za dawa ya kuzuia athari zitokanazo na kuacha matumizi ya dawa za kulevya (*Methadone*). Aidha, kazi nyingine iliyotekelezwa ni kuendesha kampeni za uhamasishaji wa kufanya mazoezi kwa kila Mtanzania mara kwa mara kama moja ya mkakati wa kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *International Centre for Eye Health* imeandaa mpango wa kuimarisha huduma za macho kwa watu wanaoishi na ugonjwa wa Kisukari zinazotolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali za Rufaa za Kanda za KCMC and Mbeya.

HUDUMA YA TIBA

Usajili na Usimamizi wa Vituo vya kutolea huduma za Afya

55. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za afya kupitia vituo vya kutolea huduma nchini vikiwemo vya Serikali, binafsi na mashirika ya dini. Hadi kufika Machi 2018, huduma za afya zimeendelea kutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya **7,437** ikilinganishwa na vituo **7,284** mwezi Juni 2017. Aidha, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya Vituo binafsi 153 vya kutolea huduma za Afya vilisajiliwa.

Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, moja ya jukumu la kipaumbele kwa Wizara ilikuwa ni kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa yatolewayo nchini. Maboresho hayo, yanalenga katika kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi ili kupunguza gharama kubwa kwa Serikali katika kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Hadi kufikia mwezi Machi 2018, idadi ya Wagonjwa waliopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi ilipungua na kufikia Wagonjwa **103** ikilinganishwa na wagonjwa **304** mwaka 2016/17. Mafanikio haya ni kutokana na maboresho yaliyofanyika katika Hospitali zilizo chini ya Wizara ambapo kwa hivi sasa zimeongezewa uwezo wa kutoa huduma za Kibingwa ambazo awali hazikuwa zikitolewa hapa nchini na hivyo kulazimu wagonjwa kupatiwa rufaa nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili zilihudumia jumla ya wagonjwa **1,090,863** ambapo wagonjwa wa kulazwa walikuwa **230,403** na wagonjwa wa nje walikuwa **860,460**.

Mchanganuo wa idadi ya wagonjwa kwa kila Hospitali umeoneshwa katika **Kiambatisho Namba 2.**

Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilihudumia jumla ya wagonjwa **333,611**. Kati ya hao wagonjwa **37,226** walikuwa wa kulazwa na Wagonjwa **296,385** walikuwa ni wa nje. Aidha Hospitali kwa kushirikiana na Serikali ya Scotland ilifanya ukarabati wa vyumba viwili vya upasuaji wa Watoto na hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma za upasuaji kwa Watoto kufikia **Watoto hamsini (50)** kwa wiki kutoka **watoto 12** kwa wiki hapo awali.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali ilifanya ukarabati wa jengo la kutolea huduma za upandikizaji wa Figo na ununuzi wa vifaa Tiba kwa ajili **huduma za upandikizaji wa figo** iliyoanza kutolewa Mwezi Novemba 2017 ambapo Mgonjwa mmoja (1) alipatiwa huduma hiyo na kwa sasa wagonjwa watano (5) wamepangwa kupatiwa huduma hii mwishoni mwa Mwezi Aprili 2018. **Hatua hii imepunguza gharama za kupandikiza figo kwa mgonjwa mmoja nje ya nchi kutoka wastani wa shilingi milioni mia 100 hadi milioni 20.**

58. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeanzisha **huduma za upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia (Cochlea implant),** hadi kufikia mwezi Machi 2018, wagonjwa sita (6) walipata huduma ya kuwekewa vifaa vya usikivu. Huduma ya

kupandikiza vifaa vya kusaidia kusikia inatolewa kwa wastani wa **shilingi milioni 36 kulinganisha na shilingi milioni 80 hadi 100 ambazo zingetumika endapo mgonjwa angepelekwa nje ya nchi.**

59. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imeanza ujenzi wa jengo maalum kwa wagonjwa wanaolipia (private wing) ambapo eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 5,400 kwa ajili ya ujenzi huo limetengwa. Jumla ya **Shilingi bilioni 4** zimeshatolewa na Serikali kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Jengo hili. Aidha, katika kuboresha utoaji wa huduma za kibingwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili imekamilisha miradi mbalimbali ambayo ilikuwa imeanza katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/17 kwa kutumia fedha zake za ndani. Miradi hii inajumuisha kukamilisha ukarabati wa Jengo kuu la upasuaji lenye vyumba 8 vya upasuaji vikiwamo vyumba viwili (2) vya kupandikiza figo. Aidha, Kazi zingine zilizokamilishwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kipindi hicho ni pamoja na kukamilisha ukarabati wa jengo la kusafisha figo ambalo kwa sasa lina jumla ya vitanda 42 vya kuchujia damu ukilinganisha na vitanda 24 mwaka 2015; kukamilisha ukarabati wa Jengo la Upasuaji wa kina mama wajawazito na kuongeza vyumba vya upasuaji kutoka vyumba viwili (2) hapo awali na kufikia vyumba 4 kwa hivi sasa; usimikaji wa *lift* mbili (2) katika majengo ya Kibasila na Mwaisela; Ukarabati na usimikaji wa mfumo wa hewa katika jengo la upasuaji wa kinywa.

60. Mheshimiwa Spika, Hospitali pia, imepokea vifaa mbalimbali vyenye thamani ya **shilingi billion 1.52** kutoka Taasisi ya "Archie Wood Foundation ya Scotland" vitakavyotumika katika jengo la huduma za Kinywa na Meno. Serikali imepeleka nchini India jumla ya Madaktari 4, wauguzi 2 wa kitengo cha Tiba ya Matumbo kwa ajili ya upandikizaji wa Ini, pamoja na mhandisi wa Vifaa Tiba. Serikali kwa kushirikiana na ubalozi wa India nchini, ilipeleka madaktari 10 na wauguzi 6 (kutoka hospitali ya Taifa Muhimbili) nchini India kwa ajili ya kozi mbalimbali za muda mfupi.

61. Mheshimiwa Spika, Hali ya upatikanaji wa dawa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili imeendelea kuwa katika kiwango cha asilimia **95**. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** huwekwa katika mfuko wa fedha za kununulia dawa (**Drug Revolving Fund**) kila mwezi ili kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa dawa. Aidha, Hospitali imeendelea na shughuli za ukusanyaji wa damu katika jamii (Blood Donation Outreach Services). Zoezi hili limepunguza kwa kiasi kikubwa sana ukosefu wa damu Hospitalini na kufanya upatikanaji wa damu salama kufikia **asilimia 79** katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi, 2018. Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa huduma ya uchunguzi na tiba kwa ugonjwa sugu wa homa ya Ini (Chronic Hepatitis B), kwa kushirikiana na "Centre for Diseases Control" (CDC) ya Marekani.

62. Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato ya Hospitali kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi, 2018 umeongezeka na kufikia kiasi cha **Shilingi bilioni 46.51** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni**

31.91 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho 2016/17. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 45.7**. Pia katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Hospitali ilitoa huduma kwa wagonjwa wa msamaha zenye thamani ya **Shilingi bilioni 3.4** ikilinganishwa na huduma zenye gharama ya **Shilingi bilioni 2.21** zilizotolewa katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2017.

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

63. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya MOI imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma ya matibabu ya mifupa, upasuaji mishipa ya fahamu na ubongo. Huduma hizi zimekuwa zikitolewa kwa weledi kwa kutumia wataalamu wazalendo. Kati ya Julai 2017 hadi Machi 2018, MOI imeshatoa matibabu ya upasuaji kwa **wagonjwa 4,001** kati yao; upasuaji mifupa wagonjwa 3,121 kubadilisha nyonga wagonjwa 120, goti wagonjwa 88, upasuaji wa uti wa mgongo wagonjwa 227, ubongo wagonjwa 94, na watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi wagonjwa 351. Aidha, mwezi Februari 2018, **Taasisi kwa mara ya kwanza imeweza kufanya upasuaji wa mgongo kwa njia ya matundu (Laparascopy) kwa kushirikiana na madaktari wa Hospitali ya BLK ya India.** Upasuaji huo ulifanyika kwa mafanikio makubwa, lengo mahsusi ikiwa ni kuwapatia weledi madaktari wa MOI ili waweze kufanya upasuaji huo.

64. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi ilikamilisha jengo la MOI awamu ya III pamoja na ununuzi wa Vifaa tiba

mbalimbali kutokana na fedha **Shilingi Bilioni 16.5** zilizopokelewa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kazi zilizofanyika ni pamoja na; kumalizia ujenzi wa jengo, Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya kutolea huduma katika Wodi za wagonjwa, Ununuzi wa mitambo na mashine zinazotumiwa kwenye vyumba vya upasuaji, Ununuzi wa vifaa tiba vya kufanyia wagonjwa mazoezi (Physiotherapy equipment), Ununuzi wa vifaa tiba vya chumba cha wagonjwa mahututi, na kitengo cha dharura, Ununuzi wa mashine za maabara, mashine za radiologia ikiwemo CT - Scan na MRI, Ununuzi wa mitambo ya hewa, kufulia umeme, na uchomaji wa taka zitokanazo na huduma za afya. Makusanyo katika Hospitali hii hadi mwezi Februari, 2018 yamefikia kiasi cha **Shilingi 10,807,695,141.93** ukilinganisha na kiasi cha **Shilingi 6,707,172,559.43** zilizokusanywa kuanzia mwezi Julai 2016 hadi mwezi Februari, 2017.

Taasisi ya Moyo - Jakaya Kikwete (JKCI)

65. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, ilihudumia jumla ya wagonjwa wenye matatizo ya moyo **42,029** kati ya hao, wagonjwa **1,440** walilazwa na wagonjwa wa nje walikuwa **40,589**. Aidha, kati ya hao wagonjwa 111, walifanyiwa upasuaji ambapo watu wazima walikuwa 52 na watoto walikuwa 59. Vilevile, Wagonjwa 157 walipatiwa matibabu kwa njia ya upasuaji wa moyo kupitia mshipa wa damu (cardiac catheterization interventions). Hivi sasa, **Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete inaweza kutoa huduma za upasuaji za ubingwa wa hali ya juu kwa asilimia 85** kwa huduma ambazo awali zilikuwa zikipatikana nje ya nchi. Hali hii imesaidia kupunguza rufaa za wagonjwa wa moyo

nje ya nchi na kuipunguzia Serikali gharama ambapo hadi kufikia Machi 2018, wagonjwa wa moyo waliopolekwa India ni **12** kutoka wagonjwa **43** kwa mwaka 2016/17.

66. Mheshimiwa Spika, Taasisi kwa kushirikiana na Madaktari rafiki wa nchini Marekani walifanya kambi maalum ya matibabu ya umeme wa moyo kwa wagonjwa wenye mapigo ya moyo ambayo yako nje ya kiwango cha kawaida kwa **kuwawekea betri maalum (pace maker)**. Jumla ya wagonjwa 11 walipatiwa matibabu kipindi cha kambi hiyo iliyofanyika mwezi Julai, 2017. Aidha, Taasisi ilipokea msaada wa vifaa vya chumba cha upasuaji ambavyo ni mashine ya usingizi na kitanda cha chumba cha upasuaji kutoka "Kuwait Fund" vyenye thamani ya **shilingi milioni 320**.

67. Mheshimiwa Spika, Taasisi kwa mara ya kwanza imefanya **upasuaji wa mishipa ya damu kwa kuunguza Laser therapy** ambapo wagonjwa wawili (2) walipatiwa huduma hii mwezi Septemba, 2017. Upasuaji huu umefanywa na Madaktari wa Taasisi kwa **asilimia 100**. Aidha, Madaktari wa Taasisi wamefanya **upasuaji wa moyo kwa kupandikiza mishipa ya moyo bila ya kusimamisha moyo (CABG off pump)** ambapo mgonjwa mmoja alinufaika na huduma hii kwa kipindi cha Julai-Desemba, 2017. Pia, Taasisi kwa kushirikiana na wataalam wa hospitali ya BLK ya nchini India ilitoa huduma za upasuaji maalum wa moyo (complex heart condition) ambapo jumla ya wagonjwa watatu walifanyiwa upasuaji mwezi Septemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, Madaktari wa Taasisi kwa kushirikiana na Madaktari bingwa kutoka USA/Italy – “Mending Kids International” walitoa huduma za kibingwa kupitia Kambi ya matibabu iliyoendeshwa mwezi Oktoba, 2017 ambapo watoto 30 pamoja na watu wazima 26 walipatiwa huduma ya upasuaji maalum wa moyo kwa kupitia tundu dogo/mishipa ya damu kutumia mtambo maalum (Cath lab). Pia, mwezi Novemba 2017, Taasisi ilifanya kambi maalumu ya upasuaji kwa watu wazima. Kambi hii ilihudumiwa na Madaktari bingwa kutoka “Saifee Hospital” ya nchini India kwa kushirikiana na Madaktari wa Taasisi ambapo jumla ya wagonjwa 14 walipatiwa matibabu haya.

68. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano na Taasisi za Kimataifa katika kutoa huduma za kibingwa, mnamo mwezi Novemba 2017, Taasisi ilifanya kambi ya upasuaji wa moyo bila kufungua kifua (Catheterization) kwa kutumia mshipa wa damu wa mkono ambapo jumla ya wagonjwa 33 walifanyiwa upasuaji huo. Aidha, katika kipindi hicho Taasisi kwa kushirikiana na Madaktari kutoka SACH nchini Israel iliendesha kambi ya upasuaji wa moyo bila kufungua kifua (catheterization) kwa watoto wadogo ambapo jumla ya watoto 18 walipatiwa matibabu hayo. Vilevile, Mwezi Februari 2018, Taasisi kwa kushirikiana na madaktari kutoka Taasisi ya “Open Heart International” ya nchini Australia iliendesha kambi ya upasuaji wa kufungua kifua kwa watoto na watu wazima ambapo jumla ya wagonjwa 16 wenye matatizo ya moyo walipata matibabu hayo na kati ya hao, watoto walikuwa tisa na watu wazima saba.

69. Mheshimiwa Spika, katika kushiriki maadhimisho ya Siku ya Moyo mwezi Septemba, 2017, Taasisi ilitoa huduma ya vipimo vya afya kwa jamii ambavyo vilihusisha upimaji wa shinikizo la damu, upimaji wa uzito, urefu, na uwiano wa uzito na urefu (BMI) na upimaji wa kiwango cha sukari mwilini ambapo jumla ya watu 800 walipatiwa huduma hizo. Kati ya hao, Watu 400 waligundulika kuwa na matatizo mbalimbali ya kiafya ikiwa ni pamoja na shinikizo la juu la damu. Aidha, Taasisi imeweza kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 8,462,092,000** Katika kipindi cha hadi Machi 2018 ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 4,105,000,000.00** kilichokusanywa katika kipindi hicho mwaka 2016.

Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI)

70. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa Saratani ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2018, jumla ya wagonjwa **46,470** walipatiwa huduma. Kati ya hao, **43,599** ni wagonjwa wa nje na **2,871** ni wagonjwa ambao walilazwa. Aidha, Taasisi imeboresha tiba za mionzi ya nje kwa kufunga kifaa kiitwacho '*multi-leaf collimator*' katika mashine ya EQ80 ambacho kimenunuliwa kwa kushirikiana na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA). Vilevile, Taasisi imenunua vyanzo vipya vya mionzi kupitia Bohari ya Dawa kwa gharama ya **shilingi 473,363,437.50**. Hatua hii imeboresha utoaji wa tiba ya mionzi ya ndani kwa kutibu **wagonjwa 70** kutoka **wagonjwa 30 kwa siku**.

71. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi imeanzisha huduma za wodi za binafsi ambayo ina vitanda **4 vya VIP na vitanda 20 vya binafsi**. Hatua hii imesaidia kuboresha huduma kwa wagonjwa wenye uhitaji huo na pia kuongeza mapato. Lengo la huduma hizi ni kuhakikisha kuwa wananchi wenye uwezo wa kuchangia gharama wanakaa katika wodi binafsi. Kukamilika kwa wadi binafsi kumechangia kuongezeka kwa makusanyo ya Taasisi, ambapo katika kipindi Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya **shilingi 86,622,300** zilikusanywa ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 40,320,000** kilichokusanywa kwa kipindi cha mwaka 2016/17. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 53**. Aidha, Taasisi imeendelea kuboresha utoaji huduma kwa kutumia mfumo wa kieletroniki uitwao INAYA na kwa sasa unatumika kwa **asilimia 80** katika sehemu za huduma. Hatua hii imewezesha upatikanaji wa huduma kuwa wa haraka zaidi na kuimarisha takwimu pamoja na kudhibiti upotevu wa mapato ya Taasisi.

72. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi imetengeneza sehemu 3 za kusubiria, ambapo wagonjwa hukaa wakati wanasubiri huduma za uchunguzi na tiba. Maeneo hayo ni katika sehemu ya **mapokezi**, sehemu ya **tiba ya mionzi** na sehemu ya Kliniki ya Bima ya Afya. Hatua hii imefanya wagonjwa kuwa na sehemu nzuri na yenye utulivu wakati wakisubiri huduma katika Taasisi. Aidha, Taasisi inaendelea **kufunga mashine za tiba mpya na za kisasa za mionzi aina ya "Linear Accelerator"**, (LINAC) 2 na 'CT Simulator' (1) ambazo zimenunuliwa kwa gharama ya **shilingi 9,500,000,000**. Mashine hizo zitaiwezesha Taasisi kutoa huduma ya matibabu ya mionzi na kupunguza muda wa wagonjwa kusubiria tiba kutoka **wiki 6** sasa kufikia **wiki 2** na kuongeza ufanisi katika

tiba inayotolewa. Vilevile, Taasisi tayari imewapeleka mafunzoni nje ya nchi watumishi 7 kwa ajili ya kuongeza ujuzi wa kutumia mashine hizo ambao ni Madaktari bingwa 2, Wataalamu wa tiba ya mionzi 2, *Medical physicist 2* na *Bio-engineer 1*.

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hali ya upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Machi 2018 ilikuwa imefikia wastani wa **asilimia 85** na kwa wagonjwa wenye saratani ya mlango wa kizazi, matiti, tezi dume, njia ya chakula (oesophagus) na ngozi upatikanaji wa dawa imeendelea kuwa **asilimia 100**. Mafanikio haya yametokana na Serikali kuendelea kuchukua juhudi za makusudi katika kuboresha upatikanaji wa dawa za saratani katika Taasisi hii. Aidha, Taasisi imeendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa katika duka la dawa la jamii la Taasisi ambapo dawa za saratani zinapatikana kwa kiwango cha **asilimia 100** kwa muda wote. Duka la Dawa la Jamii limeimarisha upatikanaji wa dawa muda wote hata kwa wagonjwa wa saratani wa kipato cha chini. Hatua hii inamaanisha kuwa endapo aina ya dawa haipatikani katika Duka la Dawa la bila malipo mgonjwa ataweza kuinunua katika Duka hili kwa gharama nafuu badala ya kuinunua kutoka maduka ya nje.

Hospitali ya Benjamin Mkapa –Dodoma

74. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa ambapo jumla ya Wagonjwa **39,527** walihudhuria na kupata matibabu. Kati ya hao, wagonjwa 38,511

walikuwa wa Nje na **1,016** walilazwa. Aidha, Hospitali imefunga na kuanza kutumia mashine na vifaa vya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ya binadamu, mashine hizo ni *MRI, CT-Scan, Mammography, General Purpose X-ray, Ultra sound* na vifaa mbalimbali vya maabara. Vilevile, jumla ya wagonjwa waliofanyiwa vipimo mbalimbali walikuwa 28,736, ikiwemo *Ultra-Sound* wagonjwa 3,745, *Plain X-Ray* wagonjwa 2,081, Mammography wagonjwa 46, *CT- Scan* wagonjwa 832, MRI wagonjwa 739, *Fluoroscopy* wagonjwa 139, OGD wagonjwa 342 na *Laboratory* wagonjwa 20,812.

75. Mheshimiwa Spika, Hospitali ilipokea msaada wa vifaa vya macho vyenye thamani ya shilingi milioni 300 kutoka shirikisho la kidini nchini Marekani liitwalo LDS pamoja na Taasisi ya matibabu ya macho iitwayo "Moran Eye Center". Aidha, Hospitali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na wafadhili hao toka nchini Marekani iliendesha Kambi ya uchunguzi na matibabu ya macho kwa siku 4 mwezi Machi, 2018 ambapo wananchi walipatiwa huduma za vipimo mbalimbali. Vilevile, wataalam watatu wapo mafunzoni katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya kupata mafunzo ya matibabu ya saratani kwa watoto wadogo. Pia, Ujenzi wa Jengo la awamu ya II unaendelea kukamilishwa ikiwa ni pamoja na kupaka rangi, ufungaji wa mifumo ya maji safi na taka, ufungaji mifumo ya umeme na mfumo wa mashine za kupoza hewa.

76. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha huduma za kibingwa, mnamo tarehe 22/3/2018, Hospitali kwa kushirikiana na TOKUSHIKAI Medical group kutoka nchini Japan, ilifanikiwa **kufanya upandikizaji figo kwa mara ya kwanza kwa mgonjwa mmoja mwenye umri wa miaka 51.** Hali ya mgonjwa inaendele vizuri na amepewa ruhusa kwenda nyumabani. Aidha, Matayarisho ya **kuanzisha huduma za upasuaji wa moyo** yapo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Vile vile Hospitali iko katika hatua za mwisho za **kuanzisha huduma ya kusafisha damu** kwa wagonjwa wa figo kwa kutumia mashine maalum (Hemodialysis). Pia, hospitali imefanikiwa kuanzisha huduma za chumba cha wagonjwa mahututi (ICU). Upatikanaji wa dawa katika hospitali ilikuwa kwa **asilimia 95.2** kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018. Uwezo wa hospitali kukusanya mapato umeendelea kuimarika ambapo jumla ya **Shilingi 1,892,978,585** kimekusanywa hadi Machi 2018 ukilinganisha na **Shilingi 794,162,415** zilizokusanywa katika kipindi cha Julai 2016 hadi Februari 2017 kwa mwaka 2016/17.

Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe

77. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mirembe na Tasisi ya Isanga imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa afya ya akili. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya wagonjwa **153,951** walipatiwa tiba pamoja na huduma nyingine za utengemao wa akili katika Hospitali ya Mirembe. Kati ya hao **124,542** walikua ni wagonjwa wa ndani (yaani wagonjwa waliolazwa na **29,409** walikua ni wagonjwa wa nje.

Aidha, wagonjwa 42 wa Taasisi ya Isanga waliruhusiwa kurudi majumbani baada ya kupitia taratibu na idhini ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kutolewa. Vilevile, kati ya wagonjwa 60 walioonwa na Bodi za Isanga, 55 wameombewa Ruhusa kwa Waziri wa Katiba na Sheria kutolewa baada ya kutimiza muda wao kisheria; mara baada ya kibali kutoka watasindikizwa makwao. Pia, katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018 Taasisi ilipokea wagonjwa 61 kwa uchunguzi na kuandikiwa taarifa za kisheria ili kuweza kusaidia mahakama mbalimbali nchini.

78. Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa dawa imeendelea kuimarika na kufikia zaidi ya **asilimia 90** kwa dawa muhimu za magonjwa ya akili. Hali ya upatikanaji wa dawa muhimu za magonjwa mengine ilikuwa zaidi ya **asilimia 80**. Aidha, hospitali imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa wa akili wa kawaida na wagonjwa wa akili walio na tuhuma za uvunjaji wa sheria kwa kuwafanyia uchunguzi, kutoa ushauri kwa mahakama, Tiba kwa umeme, Tiba kwa vikundi, Tiba kwa familia, Tiba kwa maongezi na Tiba kwa kazi (Occupational Therapy) kwa wataalamu wa kada mbalimbali ikiwemo madaktari bingwa wa afya ya Akili (Psychiatrist), Saikolojia (Clinical Psychologist), Mishipa ya fahamu (Clinical Neurologist) na wengine.

79. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, hospitali imeendelea na ujenzi wa Jengo la kuhudumia waathirika wa Dawa za kulevya lililopo chini ya Hospitali ya Mirembe katika eneo la Itega ambapo

mkandarasi yupo katika eneo husika anaendelea na kukamilisha ujenzi ili huduma zianze kutolewa mapema. Aidha, hospitali imeendelea kujenga uwezo wa Watumishi kwa kuwapeleka mafunzoni kusomea fani mbalimbali kulingana na mahitaji ya Hospitali ambapo jumla ya watumishi 12 wapo masomoni katika kada za Udaktari, Uuguzi, Fiziotherapia, Maabara na kilimo. Kati ya hao daktari bingwa mmoja ameenda Nchini Nigeria kujiendeleza na fani ya ubingwa wa hali ya juu katika kuwahudumia wagonjwa wa akili watoto na vijana. Mara baada ya kurejea Hospitali inategemea kuwa na utaalamu wa kibingwa wa hali ya juu katika kuhudumia watoto wenye shida ya akili. Vilevile, Hospitali imepokea watumishi wapya 10 wa kada mbalimbali ili kukabiliana na upungufu wa watumishi wa hospitali ya Mirembe, kati ya watumishi waliopokelewa ni wauguzi 5 na wahudumu wa afya 5.

Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu- Kibong'oto

80. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali iliendelea kutoa huduma za utambuzi na matibabu ya Kifua kikuu, Kifua kikuu sugu, VVU na magonjwa mengine ya kuambukiza. Katika kipindi hiki, Hospitali imetoa huduma kwa Wagonjwa **16,300**. Aidha kati ya Wagonjwa hao wagonjwa wa Kifua Kikuu walikuwa **235**, Kifua Kikuu Sugu (MDR-TB) wagonjwa **290**, wagonjwa wa Kifua Kikuu na Ukimwi (TB/HIV) **2,034** na Magonjwa ya kawaida wagonjwa **13,741**. Vilevile, Hospitali imeweza kutoa elimu kwa wataalamu 239 (Madaktari, wauguzi, wataalam wa maabara pamoja na wafamasia) kutoka mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuanzisha matibabu ya kifua kikuu sugu (Multi-Drug

Resistant TB, MDR TB). Pia Hospitali imeweza kuzindua jengo la kutolea huduma kwa waathirika mahala pa kazi (occupational Health Services). Pia, Wizara kwa kushirikiana na Southern African Development Community (SADC) imeanzisha huduma za afya kwa wachimbaji Madini na familia za Wachimbaji Madini.

81. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali imeanzisha huduma za Fiziotherapia kwa wagonjwa wenye mapafu yenye uwezo hafifu kutokana na TB, madhara ya vumbi kwa wachimbaji madini na matibabu mengine yanayohitaji mazoezi ya viungo. Hospitali imeweza kuhudumia wagonjwa wote wa Kifua Kikuu Sugu (DR-TB) ambao walilazwa kwa kuwapima uwezo wao wa mapafu mwanzoni mwa matibabu na kuanzisha programu ya kutibu mapafu kwa wale wenye uwezo hafifu wa Mapafu. Aidha, **hali ya upatikanaji wa dawa muhimu katika hospitali ni asilimia 90**. Vilevile hospitali imeweza kusambaza dawa za mstari wa pili za kupambana na Kifua Kikuu (second line anti TB medicine) katika mikoa yote 26 nchini ambayo ina wagonjwa wenye kifua Kikuu Sugu (MDR-TB).

Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya

82. Mheshimiwa Spika, hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya ilihudumia jumla ya wagonjwa **131,982** kutoka mikoa 7 ambayo ni Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Ruvuma, Njombe na Iringa. Kati ya hao, wagonjwa **14,982** walilazwa na wagonjwa **117,000** walikuwa ni wagonjwa wa nje. Katika kipindi cha 2017/18, Hospitali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa

kwa kuongeza miundombinu ya kutolea huduma. Ukarabati wa kupanua jengo la kutolea huduma za dharura unaendelea ambapo baada ya kukamilika kutakuwa na ongezeko la vyumba vya ushauri (consultation rooms) 3 na chumba chenye vitanda 3 kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa mahututi. Chumba cha awali kimefanyiwa maboresho na kuweza kuwa na vitanda 2 vya kuhudumia wagonjwa mahututi. Kwa ujumla hospitali itakuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa mahututi 5 kwa wakati mmoja. Aidha, eneo la mapokezi ya wagonjwa limepanuliwa kwa lengo la kupunguza msongamano wa wagonjwa na kuwapunguzia muda wa kupatiwa huduma. Vilevile, jengo la huduma za Uzazi na Mtoto (RCH) katika kitengo cha wazazi Meta limepanuliwa kwa kuongezwa vyumba vinne pamoja na sehemu ya kusubiria. Ujenzi wa wodi za watoto ulioteklezwa kwa kutumia fedha za ndani umekamilika na kuongeza vitanda vya hospitali kufikia **553** kutoka vitanda **477** vya mwaka 2016/17.

83. Mheshimiwa Spika, Katika kuboresha huduma katika hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya, Wizara inatarajia kupokea madaktari wanne (4) kutoka nchini China ambao ni wa fani za usingizi, mifupa, upasuaji wa watoto na ICU. Aidha, Upatikanaji wa dawa katika hospitali ya kanda ya rufaa Mbeya umekuwa katika kiwango cha **asilimia 95** hivyo wananchi wameondolewa usumbufu wa kufuata dawa nje ya hospitali. Aidha , Ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 yalikuwa **Shilingi 9,931,439,974.57** ukilinganisha na **Shilingi 5,607,223,511.78** kwa mwaka 2016/17.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando

84. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa, Bugando imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa kutoka mikoa 8 ya Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa ambayo ni Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Simiyu, Kigoma, Shinyanga na Tabora. Katika mwaka 2017/18, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa **128,101** ambapo wagonjwa wa nje walikuwa **108,738** na wagonjwa wa kulazwa ni **19,363**. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2018, hospitali ilifanya upasuaji kwa wagonjwa **72** wenye matatizo ya Saratani ya Utumbo mpana, saratani za tumbo, magonjwa ya pua na koo pia uti wa mgongo. Upasuaji huu ulifanywa na Madaktari wazalendo kwa kushirikiana na madaktari kutoka Marekani (Mending Kids). Pia, Hospitali imenunua Mashine ya kutibu mionzi ya ndani (Brachytherapy) kwa kushirikiana na Shirika la nguvu la Atomiki Duniani (IAEA). Kuhusu Huduma ya tiba ya saratani, jumla ya wagonjwa **131** wa saratani ya mlango wa kizazi walipatiwa huduma ya tiba ya saratani kwa njia ya mionzi (Radiotherapy).

85. Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Novemba 2017, Hospitali imeanzisha Kliniki za kibingwa ambazo zinafunguliwa baada ya masaa ya kawaida ya kazi ambapo hadi sasa, zaidi ya wagonjwa **1,000** wamehudumiwa kupitia utaratibu huo. Huduma nyingine ya Kibingwa zilizotolewa ni pamoja na usafishaji damu kwa wagonjwa wenye figo zisizo na uwezo wa kufanya kazi (Haemodialysis), ambapo jumla ya wagonjwa **48** wamepata huduma hii kwa mizunguko **1,436**. Aidha, hospitali imeendelea kuimarisha huduma ya uchunguzi wa magonjwa kwa kununua na kufunga mashine 6

mpya kwa ajili ya vipimo mbalimbali vya damu. Pia Hospitali imenunua mashine 2 za vipimo vya moyo na 1 ya ultrasound, pamoja na mashine ya **CT Scan (128 slice)** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.7** kutokana na mapato ya ndani.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC)

86. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali imeendelea kuboresha na kutoa huduma kwa wananchi wa mikoja ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga ambapo kati ya Julai 2017 na Machi 2018, jumla ya wagonjwa **143,665** walihudumiwa. Kati ya hao, wagonjwa **16,551** walilazwa na wagonjwa **127,114** ni wa nje.

87. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeweza kuhudumia wagonjwa **1,123** wa saratani ambapo wagonjwa 47 walipatiwa huduma shufaa (Palliative care). Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu kwa jamii juu ya maradhi ya saratani, Hospitali kwa kushirikiana na Taasisi ya "Mission Eine Welt" ya nchini Ujerumani, imeanzisha kampeni maalum ijulikanayo kama PrevACamp yaani *Prevention and Awareness Campaign* yenye lengo la kutoa elimu juu ya saratani, kuainisha mila na imani potofu na kufanya uchunguzi wa viashiria vya awali vya saratani. Kampeni hii ilianza Mwezi Oktoba 2017 kwa kambi ya wiki moja ya uchunguzi iliyofanyika katika hospitali ya KCMC ambapo jumla ya wananchi **1,006** (wanawake **915** na wanaume **91**) walijitokeza kufanyiwa uchunguzi wa awali na mwezi Februari 2018 ilifanyika Kambi nyingine huko Machame ambapo jumla ya wananchi **300** (wanawake **232** na wanaume **68**) waliweza kufanyiwa uchunguzi wa awali wa viashiria.

88. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali imeboresha huduma ya Afya ya Kinywa na Meno kwa kununua viti maalum vya wagonjwa na mashine maalum za X-ray za kinywa. Aidha, hospitali imeongeza vyumba vya kutolea huduma kutoka vitatu (3) vya awali hadi vitano (5). Vilevile, hospitali imendelea kutoa huduma ya kusafisha damu kwa kutumia mashine (Hemodialysis), ambapo jumla ya wagonjwa **107** (wanaume 74 na wanawake 33) wamehudumiwa ambapo jumla ya mizunguko **1,865** ya usafishaji wa damu kwa kutumia figo bandia ilifanyika kwa wagonjwa hawa. Pia, hospitali kwa kushirikiana na Shirika la Msamaria Mwema (GSF), Hospitali imefungua duka jipya la dawa na hivyo kuwezesha upatikanaji wa dawa muhimu kwa wagonjwa.

Hospitali za Rufaa za Mikoa

89. Mheshimiwa Spika, Uendeshaji wa Hospitali za Rufaa za Mikoa ulikuwa unasimamiwa na kuratibiwa na OR-TAMISEMI. Hata hivyo, baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa tarehe 25 Novemba 2017, usimamizi na uendeshaji wa Hospitali hizi sasa upo chini ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Hospitali za Rufaa za Mikoa zilizopo ni 28.

90. Mheshimiwa Spika, Pamoja na huduma za matibabu za kawaida, Hospitali za Rufaa za Mikoa hutoa huduma za kibingwa ambazo hazitolewi katika hospitali ngazi ya Halmashauri/Wilaya. Huduma muhimu za kibingwa zinazopaswa kutolewa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ni pamoja na: Upasuaji (General Surgery),

Magonjwa ya Wanawake na Uzazi (Obstetrics & Gynaecology), Magonjwa ya Watoto (Paediatrics & Child Health), Magonjwa ya ndani (Internal Medicine), Magonjwa ya Kinywa na Meno (Dentistry) na Radiolojia (Radiology). Wizara imeweka mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na mrefu ili kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa katika Hospitali hizo zinaboreshwa. Mikakati hiyo ni pamoja na **kuboresha miundombinu ya kutoa huduma, kuongeza idadi ya madaktari bingwa, kuboresha upatikanaji wa dawa**, kupanga kwa uwiano watumishi wa Hospitali za Rufaa za Mkoa kwa kuzingatia huduma na uzito wa kazi zinazotolewa na hospitali hizo, kuanzisha na kuboresha huduma za afya kwa njia ya masafa (**telemedicine**) kwa kila Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na kufanya huduma hiyo kutumika kama kiunganishi kati ya Hospitali hizo na Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa, kuboresha utoaji wa huduma za uchunguzi wa maabara na radiolojia kwa kupanua na kuimarisha miundombinu ya huduma za uchunguzi ikiwa ni pamoja na kununua na kuweka vifaa vya kisasa vya maabara na radiolojia.

91. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Hospitali za Rufaa za Mkoa (28) zilihudumia jumla ya wagonjwa **1,637,835** ambapo wagonjwa wa nje walikuwa **1,329,364** na wagonjwa wa ndani walikuwa **308,471** kama inavyooneshwa kwenye **kiambatisho namba 3**

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza (NCDs)

92. Mheshimiwa Spika, Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kumekuwa na ongezeko la Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza hapa nchini. Utafiti wa viashiria vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza uliofanywa na Wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya utafiti wa magonjwa ya binadamu (NIMR) mwaka 2012, ulionesha kuwa kuna ongezeko kubwa la viashiria vinavyosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Utafiti huo ulionesha kuwa asilimia 15.9 ya wananchi wanavuta sigara, asilimia 29.3 wanakunywa pombe, asilimia 97.2 wanakula mboga mboga na matunda chini ya mara tano kwa wiki. Aidha utafiti ulionesha kuwa, asilimia 26 ya wananchi ni wanene kupita kiasi, asilimia 26 wana lehemu nyingi mwilini, asilimia 33.8 wana mafuta mengi mwilini, asilimia 9.1 wana kisukari na asilimia 25.9 wana shinikizo kubwa la damu. Utafiti pia ulionesha kwamba, asilimia 25 ya wananchi waliohojiwa hawajishughulishi na kazi zinazotumia nguvu na hawafanyi mazoezi yeyote.

93. Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza yamekuwa yakiendelea ndani ya Wizara yangu na yamejikita zaidi katika masuala ya Kinga, kama tunavyofahamu kuwa **Kinga ni bora kuliko Tiba**. Tangu kuanzishwa kwa kampeni ya **"Afya Yangu Mtaji Wangu"** ilizinduliwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara imeendelea kuhimiza jamii kuhusu umuhimu wa kufanya mazoezi mara kwa mara sambamba na kujiepusha na visababishi vingine vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo ulevi kupita kiasi na uvutaji wa sigara na

tumbaku. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Wadau kufanya Kampeni za uchunguzi wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza katika Mikoa yote. Nitumie fursa hii kulipongeza Bunge lako tukufu kwa kuanzisha Jukwaa la Waheshimiwa Wabunge la Kupambana na Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza ili waweze kupata elimu namna ya kujikinga na Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza na kuwaelimisha wananchi juu ya magonjwa hayo.

94. Mheshimiwa Spika, Kuhusiana na suala la kupambana na athari za matumizi ya madawa ya kulevya, tunavyo jumla ya vituo 5 nchini kwa sasa vinavyotoa matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevya kwa kutumia dawa ya *Methadone*. Vituo hivi vipo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Mwananyamala na Temeke (Mkoa wa Dar es Salaam), Itega (Dodoma), Hospitali ya Sekou Toure (Mwanza) na Hospitali ya Rufaa Mbeya. Hadi kufikia Machi 2018, vituo hivi vilikuwa vimesajili waathirika wa dawa za kulevya wapatao **5,560**. Pamoja na kutibu uraibu, vile vile vituo hivi vinatoa matibabu ya magonjwa yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile VVU/UKIMWI, Kifua kikuu, Homa ya ini (Hepatitis B na C) pamoja na magonjwa mengine yanayowapata watumiaji wa dawa za kulevya. Kwa sasa, dawa ya *Methadone* inapatikana katika mfumo rasmi wa ununuzi, Utunzaji na Usambazaji kwa kutumia Bohari ya Dawa (MSD). Hatua hii, inasaidia kuhakikisha kuwa vituo vyote vilivyofunguliwa na vitakavyo funguliwa vitapata dawa ya kutosha na kwa wakati.

Upatikanaji wa Damu Salama

95. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa damu salama, Mpango wa Taifa wa Damu Salama umeendelea kukusanya, kuhifadhi na kusambaza damu salama katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018 Mpango ulifanikiwa kukusanya idadi ya chupa za damu **233,953** ambazo ni sawa na **asilimia 101** ya lengo la makusanyo kwa mwaka ambalo lilikuwa ni kukusanya chupa za damu **230,000**. Aidha, chupa zote za damu (**233,953**) zilizokusanywa zilipimwa makundi ya damu pamoja na magonjwa makuu manne ambayo ni UKIMWI (HIV), Homa ya ini (HBV &HCV) na kaswende (syphilis) kabla ya kugawa kwenye vituo vya kutolea huduma kabla ya kuzitoa kwa wahitaji. **Nitumie Bunge Iako Tukufu kuwashukuru wananchi wote wanaojitolea kuchanga damu. Aidha nitoe rai kwa watanzania kuchangia damu mara kwa mara ili kuokoa maisha ya wagonjwa hasa wanawake wajawazito na watoto wa umri chini ya miaka 5.**

Huduma za uchunguzi wa Magonjwa

96. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha huduma za maabara ambapo hadi kufikia mwezi Agosti 2017, jumla ya maabara 76 kutoka maabara 66 katika mwaka 2016 ambazo zipo katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Vituo vya Afya, zilishiriki kwenye utaratibu wa Shirika la Afya Duniani wa kutoa Ithibati hatua kwa hatua, na kupewa nyota za viwango vya ubora wa huduma za maabara. Maabara **33** ziliweza kupata kuanzia nyota moja (**1**) mpaka nne (**4**) za viwango vya ubora. Aidha, Maabara za Taifa,

Kanda, Maalum na zile za Binafsi kumi **(10)** zimepata ithibati ya SADCAS ya kiwango cha kimataifa yaani **ISO 15189:2012**. Maabara hizo ni Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (NHLQATC), Hospitali ya Kanda Bugando (BMC), Hospitali ya Kanda Mbeya (MRH), Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC), Hospitali ya Mnazi Mmoja (Zanzibar), Hospitali ya Aga Khan, Maabara ya Lancet, Hospitali ya Mission Ndanda na Hospitali maalum ya Kibong'oto. Pia, Wizara inaendelea na ujenzi wa maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii katika eneo la Mabibo, Dar es salaam. Mradi huu hadi kukamilika unatarajiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 7,493,193,434.97.00**, zinazotolewa na Benki ya Dunia.

97. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuboresha huduma na ubora wa vipimo katika maabara za tiba na afya ya jamii. Kupitia Maabara kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii, serikali imeendelea kuimarisha ubora wa vipimo vya VVU katika vituo vinavyotoa huduma hii nchini kwa kuhakikisha vinapelekewa vipimo vya uhakiki wa ubora, kutoka 4,500 hadi 5,400 kutoka mwaka 2017 hadi 2018 na tunatarajia kuongeza vituo vingine 600 kabla ya mwisho wa mwaka 2018. Pia katika mpango huu wa kuhakiki ubora zaidi ya matoleo 80 ya vitendanishi vya kupima VVU na Malaria yamefanyiwa uhakiki kabla ya kusambazwa kwa watumiaji nchini kwa kipindi cha mwaka 2017/18.

98. Mheshimiwa Spika, ili kupambana magonjwa ya mlipuko serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha upimaji wa magonjwa ya

mlipuko, ikiwemo kuimarisha mfumo wa kusafirisha sampuli nchini, kutoa mafunzo kwenye maabara za Rufaa za Mikoa zilizoko mikoa ya mipakani katika utambuzi wa magonjwa ya Mlipuko, ambapo maabara 11 zimewezeshwa kupima na kutambua magonjwa ya mlipuko na usugu wa vimelea vya magonjwa. Utaratibu huu utaendelea kwa awamu kwa maabara nyingine zilizobakia ili kuhakikisha kuwa maabara zote zinapata uwezo huu. Aidha, maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (Public Health Laboratory) inayojengwa na serikali katika eneo la Mabibo (Dar es Salaam) itasaidia kuboresha huduma za uchunguzi wa Magonjwa ya mlipuko. Maabara hii itafanya kazi kwa kushirikiana na Maabara kuu ya Taifa pamoja na ile iliyopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya katika kudhibiti magonjwa haya. Vilevile, Serikali kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ushirikiano na serikali ya Ujerumani inatarajia kuanzisha maabara 3 zinazohamishika, hali itakayosaidia ugunduzi wa magonjwa katika maeneo husika kwani tutaweza kutumia gari maalum iliyobeba vifaa vya maabara hadi eneo la tukio la mlipuko na hivyo kuharakisha uchunguzi, tiba na njia nyingine za kinga.

99. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuboresha na kutoa huduma za **uchunguzi wa magonjwa kwa njia ya Radiolojia** katika hospitali zenye mashine hizo za uchunguzi (Ultrasound, X-ray, CT, MRI). Vilevile, Serikali imeandaa Mwongozo wa vifaa vya radiolojia nchini (Standard Medical Radiology and Imaging Equipment Guidelines). Aidha, Wizara inakamilisha taratibu za kupokea mashine za kidijitali 34 kutoka kampuni ya Philips ambapo Awamu ya Kwanza itahusisha Hospitali kumi (10) za Umma za Rufaa za Mikoa ya **Manyara, Kagera,**

Ruvuma, Singida na ya Halmashauri za **Nzega, Magu, Mpanda, Songwe, Njombe na Bariadi.**

100.Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuboresha **huduma za ufundi wa vifaa na vifaa tiba** kwa kuwa zina umuhimu mkubwa katika utoaji wa huduma za Afya katika ngazi zote. Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Korea kupitia taasisi ya KOFIH ilitoa mafunzo ya ujuzi wa kufanya matengenezo ya vifaa vyenye teknolojia za kisasa ikiwa ni pamoja na vifaa vya chumba cha upasuaji, Maabara, Utakasishaji, Radiolojia, Wodi ya Wazazi, dharura na wodi ya wagonjwa mahututi kwa mafundi 30 wa vifaa tiba kutoka katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali Tatu (3) za kanda, Hospitali 2 za tiba maalum, Hospitali Nne(4) za mikoa, Hospitali Saba (7) za Wilaya, Hospitali mbili (2) za Jeshi(JWTZ 1 na Polisi 1), Bohari ya Dawa (MSD) na vyuo viwili (2).

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

101.Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua mchango wa huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala katika utoaji wa huduma za afya nchini. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018, Serikali imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali kupitia njia za mitandao ya kijamii, magazeti, radio na runinga. Aidha, Wataalam na watafiti **24** wa Tiba Asili kutoka Taasisi za ITM-MUHAS, NIMR na GCLA wamekuwa wakipata mafunzo kutoka kwa wataalam **watatu (3)** kutoka Jamhuri ya Watu wa China kuhusu namna bora ya kutafiti na kutengeneza dawa za asili. Vilevile, Waganga wa tiba asili **107** walipata elimu kuhusu **usajili wa dawa** za asili, na kwa kushirikiana na ITM-

MUHAS, waganga **25** wa tiba asili walipata mafunzo ya muda mfupi (siku 7) kuhusu namna bora ya kuandaa dawa za asili.

Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

102.Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara yangu imeendelea kuhakikisha kwamba hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma inaendelea kuimarika. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kuimarika hadi kufikia wastani wa **asilimia 81** kwa Dawa muhimu 135. Aidha, katika kipindi hicho, hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo ilifikia **asilimia 92 kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini**. Vilevile, kutokana na kuendelea kuwasili kwa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo nchini, na kwa mujibu wa mikataba iliyopo kati ya wazalishaji na Bohari ya Dawa, hali ya upatikanaji wa dawa kwenye hospitali inatarajiwa kuimarika na kufikia asilimia 89 ifikapo mwishoni mwa mwezi Aprili 2018.

103.Mheshimiwa Spika, katika kupunguza gharama za ununuzi wa Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuongeza upatikanaji wake, Wizara kupitia Bohari ya Dawa imeingia Makubaliano ya muda mrefu (Framework Agreement) na wazalishaji wa dawa 110 na kati ya hao 10 ni wazalishaji wa ndani. Aidha, hatua hii imesaidia kupunguza bei ya dawa kwa wastani wa **asilimia 40**, ukilinganisha na bei ya zamani ya mawakala au washitiri wa kawaida kabla ya utaratibu wa kununua dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji. Vilevile, hadi kufikia Machi 2018, Wizara ilikuwa

imepokea Jumla ya **Shilingi 70,940,858,412** kwa ajili ya ununuzi wa dawa Vifaa, Vifaa Tiba na chanjo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 59,917,232,844.00** ni kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na **Shilingi 10,838,846,362.00** kwa ajili ya ununuzi wa chanjo.

104.Mheshimiwa Spika, mbali na kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, matumizi yasiyo sahihi ya dawa yamezidi kuongezeka hasa matumizi yasiyo ya lazima ya dawa aina ya antibiotiki na uchomaji wa sindano usiokuwa wa lazima. Aidha, tabia ya baadhi ya wagonjwa kwenda moja kwa moja kwenye maduka ya dawa na kununua dawa bila ushauri wa daktari wala kuwa na cheti cha dawa imeendelea kuongezeka na hivyo kuathiri matumizi sahihi ya dawa nchini. Vilevile, baadhi ya wagonjwa kusitisha matumizi ya dawa kabla ya muda sahihi wa matumizi pale tu wanapojisikia wamepata unafuu.

105.Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wizara yangu ilifanya yafuatayo:

- i. Kuandaa Mkakati wa uhamasishaji Jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa nchini (Communication Strategy To Promote Rational Use of Medicines to the Community)
- ii. uzinduzi Mpango wa Taifa wa kupambana na usugu wa dawa aina ya *antimicrobials* (National Action Plan on antimicrobial resistance) na unaendelea kutekelezwa.
- iii. Kupitia Kitengo cha Huduma za Dawa (PSU) Wizara

ilishiriki katika vipindi mbalimbali vya Radio na Runinga katika kuelimisha Jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa.

- iv. Kamati za Dawa na Tiba zimeundwa katika Hospitali zote nchini ili kusimamia matumizi sahihi ya dawa. Vilevile, kamati za Uendeshaji za vituo vya Afya na Zahanati zimeendelea kuhimizwa kusimamia matumizi sahihi ya dawa katika maeneo yao.

106. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuanzisha viwanda vya dawa Nchini ili kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji iliweza kuandaa mkutano mkubwa kwa lengo la kuwaleta pamoja wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika viwanda vya dawa na vifaa tiba. Jumla ya wadau mia nne thelathini **(430)** walihudhuria mkutano huo na wawekezaji thelathini na nane **(38)** walijitokeza kuwekeza katika uzalishaji wa dripu (*infusion*), uzalishaji wa bomba za sindano, uzalishaji wa vifungashio vya dawa, uzalishaji wa bidhaa za pamba zinazotumika hospitalini, uzalishaji wa dawa za kuhifadhi maiti. Aidha, Serikali imeweka utaratibu maalumu wa kuwafuatilia wawekezaji hawa walionyesha nia ili kuhakikisha wanafanikiwa katika azma yao ya kuwekeza. Serikali itaendelea kuhakikisha inatoa fursa ya soko la kutosha kwa dawa na vifaa tiba vitakavyozalishwa hapa nchini kwa kutenga bajeti ya kukidhi mahitaji ya dawa na vifaa tiba nchini. Uwepo wa Viwanda hivyo utawezesha Serikali kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza dawa toka nje ya nchi. Jitihada hizi zitasaidia kuongeza uzalishaji wa ndani ambao kwa sasa hivi ni asilimia 6

hivyo na kupunguza kiwango cha uagizaji wa dawa nje ya nchi ambao kwa sasa ni asilimia 94.

UHAKIKI UBORA WA HUDUMA ZA AFYA

107.Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya Uhakiki na Ukaguzi kwa vituo vya kutolea huduma za Afya. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara ilifanya zoezi la tathmini ya mara ya pili (re-assessment) ya kutoa nyota kulingana na ubora kwa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya ya Msingi (Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali katika Halmashauri/Wilaya) katika mikoa 14 ya Dar es Salaam, Iringa, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mwanza, Pwani, Tanga, Tabora, Singida, Simiyu na Shinyanga. Jumla ya Vituo **3,856** vilipewa hadhi ya nyota kulingana na ubora wa huduma zinazotolewa. Vigezo vinavyotumika kupima ubora wa huduma ni pamoja na uongozi wa kituo, upatikanaji wa dawa, utendaji kazi wa watumishi, ubora wa huduma za maabara, ushirikishwaji wa wananchi, huduma za tiba ya dharura na rufaa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na matumizi ya takwimu. Katika matokeo ya tathmini ya awali ya mwaka 2016, jumla ya vituo **1,244** sawa na **asilimia 33** ya vituo vyote **3,713** vilivyofanyiwa tathmini ya ubora katika mikoa **vilipata nyota sifuri** na vituo **62** sawa na **asilimia 2 vilipata nyota 3 au zaidi**, ukilinganisha na tathmini ya mara ya pili iliyofanyika mwaka 2017/18 katika mikoa 14, ambapo vituo 180 sawa na **asilimia 4.7 tu ndivyo vimepata nyota sifuri na Vituo 749 sawa na asilimia 19.4 vilipata nyota 3 na zaidi**. Matokeo haya ya tathmini ya pili yameonesha kuimarika kwa ubora wa huduma katika vituo hivyo, ambako ndio

wananchi wengi wanapata huduma kama ilivyochambuliwa katika **Kiambatisho Na 4** limefafanua zaidi.

108. Mheshimiwa Spika, Mipango ya Uimarishaji Ubora wa huduma za afya kwa kila Kituo iliandaliwa na utekelezaji unaendelea kwa kushirikiana na Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri. Aidha, Wizara imekamilisha Mwongozo wa viwango vya kutolea huduma katika hospitali za rufaa ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa. Kwa kutumia viwango hivi, tayari tathmini imefanyika katika Hospitali za Rufaa za mikoa ya Mbeya, Tanga, Lindi, Mtwara, Kigoma, Kagera, Geita, Mara, Mwanza na Shinyanga ili kupima Ubora wa Huduma za Afya katika hospitali hizo. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa Hospitali nne (Geita, Kigoma, Mara na Shinyanga) zimepata nyota moja na hospitali sita (Kagera, Lindi, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Tanga) zimepata nyota mbili. Mikoa iliyobaki inaendelea kufanyiwa tathmini. Maeneo yaliyoonekana kuwa na changamoto ni ukosefu wa wataalam bingwa, huduma za tiba za dharura, huduma za wagonjwa mahututi na huduma za upasuaji. Mipango ya Uimarishaji Ubora wa huduma za afya kwa kila Hospitali iliandaliwa na utekelezaji unaendelea kwa kushirikiana na Timu za Menejimenti za Hospitali husika.

109. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeendelea na maandalizi ya kuanzisha huduma za dharura katika barabara kuu. Huduma hizi zitatekelezwa chini ya udhamini wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa Southern Africa Trade and Transport Facilitation (SATTF) unaosimamiwa na TANROADS. Maandalizi hayo yamehusisha

ununuzi wa magari ya kubebea wagonjwa (ambulances) **12**, mabasi madogo mawili ya wagonjwa (rider vans) na magari ya uokoaji **5** yenye uwezo wa kuinua magari yaliyopata ajali na kukata vyuma (rescue vans). Vilevile imewezesha kununua vifaa vya mawasiliano pamoja na vifaa tiba na vifaa vya kufundishia wataalam wa dharura. Aidha, Wizara imeandaa michoro ya vituo vya kutolea huduma katika barabara kuu vitakavyojengwa na kutumika katika awamu ya kwanza inayohusisha barabara kutoka Dar es salaam hadi Ruaha Mbuyuni. Vilevile, kupitia ufadhili wa *Bloomberg Initiative on Global Road Safety*, Wizara imetoa mafunzo kwa Waandishi na Wanasheria kuhusu masuala ya Usalama Barabarani ambapo viashiria vitano vinavyoongoza kwa kusababisha ajali za barabarani na madhara yake ambavyo ni kutokuvaa mikanda, kutokuvaa kofia ngumu, kutomkalisha mtoto kwenye kiti maalum, kunywa pombe na kuendesha gari na mwendokasi vinafanyiwa kazi.

Ushirikiano wa Ndani na Nje ya Nchi

110. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi rafiki pamoja na Jumuiya mbalimbali katika masuala ya Afya. Wizara iliratibu ushiriki katika mikutano ya Jumuiya mbalimbali za Kikanda na Kimataifa, kwa nia ya kuimarisha utoaji wa huduma katika Sekta ya Afya ambapo Wizara iliandaa na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Afya Jumuiya ya Nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Africa (ECSA-Health Community) uliofanyika nchini, Mwezi Machi 2018. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano kupitia jumuiya za kikanda ikiwemo SADC,

EAC, African Union, Great Lakes Initiative Africa (GLIA) na ECSA-HC pamoja na ushirikiano na nchi marafiki (bilateral cooperations) kupitia *Joint Permanent Commissions* (JPCs).

RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

111. *Mheshimiwa Spika*, Katika kuongeza idadi ya wataalamu wa Afya nchini, Wizara imeendelea kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi NACTE katika kusimamia ubora wa mafunzo ya kada za Afya zisizo katika kiwango cha shahada. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya wanafunzi **16,214** walichaguliwa kujiunga na vyuo vya Afya. Kati ya hao wanafunzi **6,564** walichaguliwa kwenye vyuo vya Serikali na **9,650** kwenye vyuo binafsi katika programu za Uuguzi na Ukunga, Sayansi Shirikishi za Afya na wahudumu Afya ya Jamii. Aidha, Jumla ya wanafunzi **23,098** walifanya mitihani ya kuhitimu katika kipindi hiki, kati yao **10,669** ni wa Sayansi Shirikishi za Afya, **7,300** wa Uuguzi na Ukunga na wa Wahudumu Afya ya Jamii **5,129**.

112. *Mheshimiwa Spika*, Katika usimamizi wa mafunzo ya kada za afya zisizo katika kiwango cha shahada nchini, Wizara inao utaratibu wa kutathmini watahiniwa wote kwa usawa kwa kusahihisha mitihani ya kitaifa kwa pamoja (central marking). Katika mwaka 2018, jumla ya watahiniwa **14,477** kutoka kwenye vyuo 177 vya Serikali na vyuo binafsi wamesahihishiwa mitihani yao na kupewa matokeo. Miongoni mwa watahiniwa, watahiniwa **10,669** ni wa kada ya Sayansi shirikishi za Afya na **3,808** fani za Uuguzi na Ukunga. Pia, jumla ya wakufunzi **139** kutoka vyuo **93** vya Uuguzi na Ukunga

walifundishwa mbinu ya kutumia mitaala iliyohuishwa kwa mwaka wa masomo 2017/18.

113. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa Maendeleo katika kutoa ufadhili wa mafunzo ya kibingwa ya muda mfupi na muda mrefu yanayolenga kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wa sekta ya Afya. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 jumla ya **Watumishi 376** wameendelea kulipiwa gharama za masomo yao ndani na nje ya nchi katika ngazi ya shahada ya Uzamili hususan Madaktari Bingwa katika fani za kipaumbele za upasuaji, magonjwa ya wanawake na uzazi, magonjwa ya watoto, magonjwa ya ndani na radiolojiawe.

114. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2017/18 ,Wizara yangu, ilipokea kibali cha ajira ya watumishi **3,152** wa kada za afya kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kibali hicho kilikuwa na nafasi za Madaktari Daraja la II **45**, Madaktari Bingwa (Medical Specialist) **24**, Madaktari Washauri (Medical Consultant) – **2**, Wauguzi Daraja la II **137** na kada nyingine za Afya **3,081** ambapo mchakato mzima wa kujaza nafasi za ajira ambazo Wizara ilipewa ulikamilika na Watumishi wote walipatikana isipokuwa Madaktari Washauri. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishawapangia Vituo vya kazi Watumishi hao. Aidha Katika kipindi hiki jumla ya Wataalam wa kigeni **35** walipata ajira katika taasisi mbalimbali za Serikali.

115. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, imeendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi ambao wanafanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuwapatia motisha ili kuendelea kutoa huduma za afya katika maeneo hayo. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018 jumla ya nyumba 30 zimejengwa na kukamilika katika Halmashauri tatu (3) za mkoa wa Manyara, ambazo ni ; Halmashauri za Kiteto 10, Simanjiro 10 na Hanang nyumba 10. Kukamilika kwa nyumba hizo kumeongeza idadi ya nyumba za watumishi zilizojengwa kupitia mradi huu wa 'Global Fund' na kufika nyumba **480** katika maeneo yenye mazingira magumu.

UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA

116. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya inaendelea na utekelezaji wa mpango wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Hadi kufikia Machi 2018 Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulikuwa na jumla ya kaya **2,096,692** zilizojiunga ukilinganisha na kaya **2,030,666** zilizokuwa zimejiunga mwaka 2016/17. Aidha, wanufaika wameongezeka kutoka **12,183,996** mwaka 2016/17 hadi kufikia wanufaika **12,580,149** Machi 2018 sawa na **asilimia 25** ya Watanzania wote. Vilevile, katika kuchangia juhudi za wananchi wanaochangia CHF na kuboresha huduma zitolewazo, Serikali hutoa malipo ya tele kwa tele kwenye Halmashauri kulingana na kiwango cha makusanyo ya CHF. Malipo yaliyofanyika kwa Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018 ni **Shilingi bilioni 1.4.** na hivyo kuwezesha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kulipa

malipo ya Tele kwa Tele yenye jumla ya **Shilingi bilioni 15.8** kwa Halmashauri mbalimbali nchini tangu Mfuko ulipokabidhiwa jukumu hili mwezi Julai 2009.

117. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza idadi ya wananchi watakao kuwa wanahudumiwa na Mfuko huo, Wizara yangu kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI imejipanga kuanza kutekeleza CHF iliyoboreshwa (iCHF) kabla ya mwisho wa mwezi Aprili, 2018. Katika maboresho hayo kila mwanachama ataweza kupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa bila kujali Kituo/Halmashauri alipojisajili tofauti na ilivyo sasa ambapo mwanachama wa CHF hupata huduma kwenye zahanati hadi ngazi ya Hospitali ya Wilaya/Halmashauri aliyojisajili tu.

118. Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za kuhakikisha inafikia malengo ya afya kwa wote (Universal Health Coverage) ambapo kila mwananchi atakuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma bora za afya bila kuwa na kikwazo cha kifedha. Lengo ni kuwa ifikapo mwaka 2020 **asilimia 70** ya wananchi wawe wamejiunga na mifuko ya Bima ya Afya. Hali iliyopo sasa inaonesha kuwa idadi kubwa ya wananchi takribani **asilimia 68** nchini wapo nje ya Mfumo wa Bima ya Afya. Hii ina maana kuwa ni takribani ya **asilimia 32** ya watu wote ndiyo waliopo katika mfumo wa Bima za Afya nchini. Kwa hali hiyo, watu wengi nchini bado hawana uhakika wa kupata huduma za afya pindi wanapozihitaji kutokana na kuwa nje ya mfumo wa bima ya afya. Ili kuhakikisha kuwa wananchi hawa wanalindwa (Social protection) na athari hizo,

Serikali iko katika hatua za kuboresha Mfumo wa Bima ya Afya kwa kuweka mazingira yatakayohakikisha kila mwananchi anapata huduma bora za afya pindi anapozihitaji. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara iliandaa na kuwasilisha Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye maelekezo ya kuboresha mfumo wa Bima za Afya nchini ikiwa ni pamoja na kutunga Sheria itakayomtaka kila Mtanzania kujiunga katika Mfumo wa Bima ya Afya. Baada ya kuwasilishwa kwa Rasimu hiyo, ulitolewa ushauri na maelekezo ambayo Wizara tayari imeshayafanyia kazi na tayari imeshaandaa rasimu nyingine ya Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye kuzingatia ushauri ambao Wizara ilipatiwa. Rasimu ya Waraka huu unatarajiwa kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi ndani ya Serikali kabla ya kuandaliwa kwa muswada wa sheria utakaowasilishwa bungeni kwa dhamira ya kutunga sheria itakayomtaka kila mwananchi kuwa mwanachama wa mfuko wa Bima ya Afya.

Mfuko wa Afya wa pamoja (Health Basket Fund)

119. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea na jukumu la kuratibu Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund) ulioanzishwa mwaka 1996. Kupitia Sekretarieti ya Uratibu wa Mfuko, vikao mbalimbali vya majadiliano kati ya Serikali na Wadau vimekuwa vikifanywa ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya Serikali jinsi inavyotekeleza kazi zinazogharamiwa na fedha za Wadau. Kwa hivi sasa mfuko huo unachangiwa na Wadau (7) ambao ni Denmark, Uswisi (SDC), Ireland, Canada, Benki ya Dunia, UNICEF na Korea Kusini.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, kiasi cha **shilingi 26,674,357,344.00** kimepokelewa kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 22,278,604,900.00**, sawa na asilimia 90 ya fedha zote zilipokelewa zilipelekwa na kutumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuboresha huduma za afya ngazi ya msingi. Fedha hizi hutumika kwa mujibu wa Mkataba wa Makubaliano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo, ambapo **asilimia 33** ya fedha zinazopelekwa katika Halmashauri zinatakiwa kutumika kama nyongeza ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na **asilimia 67** ni kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali ambazo zinalenga katika kuboresha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kugharamia usambazaji na ufuatiliaji wa chanjo kwa kuimarisha mnyororo baridi (cold chain), uimarishaji wa huduma za dharura za mama na mtoto (CEmOC), udhibiti wa magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza pamoja na yale yasiyopewa kipaumbele na kuwajengea uwezo watoa huduma za afya.

120. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeanza utekelezaji wa azimio la kupeleka fedha moja kwa moja katika Vituo vya kutolea huduma za Afya nchini (Direct Health Facility Financing (DHFF) badala ya kuzipeleka kwenye Halmashauri zao. Hatua hii imelenga kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha za afya na kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Utekelezaji wa azimio hili umeanza katika kipindi cha 2017/2018 ambapo fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya

vituo vya kutolea huduma za Afya zilipelekwa moja kwa moja kutoka Hazina kwenda katika Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Jumla ya **shilingi 45,751,004,800** zimetolewa na kupelekwa katika vituo **5,170**. Hatua hii imechangia kuboresha upatikanaji wa fedha katika vituo kwa wakati na kusaidia vituo kupanga mikakati ya kuboresha huduma na kuleta ufanisi.

Malipo kwa Ufanisi (Results Based Financing- RBF)

121. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza Mpango wa Malipo kwa ufanisi ambao ni ubunifu unaolenga kuongeza uwajibikaji wa Watoa huduma za afya pamoja na kuboresha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuboresha upatikanaji na utumiaji wa huduma za afya nchini. Utekelezaji wa Mpango wa malipo kwa ufanisi hupimwa kwa viashiria muhimu hasa vya afya ya mama na mtoto, ambavyo hulipwa kwa kazi inayofanyika baada ya uhakiki wa takwimu za viashiria hivyo. Msingi Mkuu wa mpango huu ni kwamba: "*fedha hulipwa kutokana na idadi ya wagonjwa/wateja na huduma bora iliyotolewa.*" Kadri kituo cha kutolea huduma za afya kinavyovutia zaidi wagonjwa na kutoa huduma bora ndivyo kitakavyopokea zaidi motisha kwa kituo na kwa watumishi. Pia, vituo vinapewa madaraka ya namna ya kupanga na kutumia mapato yatokanayo na fedha wanazopata.

122. Mheshimiwa Spika, Mpango huu kwa hivi sasa unatekelezwa katika Mikoa minane (8) ambayo ina kiwango kikubwa cha vifo vya akinamama na watoto ambayo ni Kigoma, Geita, Kagera,

Shinyanga, Mwanza, Tabora, Simiyu & Pwani. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya **Shilingi 35,917,673,288.88** zimepelekwa katika Mikoa (RHMT), Mamlaka za Serikali za Mitaa (CHMT) na vituo vya kutolea huduma za Afya (Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati) kwa ajili ya uboreshaji wa Miundombinu ya kutolea huduma za afya na malipo ya motisha kwa watumishi wa ngazi ya Mkoa (RHMT), ngazi ya Wilaya (CHMT), watoa huduma za Afya katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati.

Uimarishaji wa Mifumo ya Afya nchini

123. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Kitengo cha Kuimarisha Mifumo ya Afya nchini (HSS) unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia 'Global Fund' imeendelea, kutekeleza shughuli mbalimbali za Uimarishaji wa Mifumo ya Afya. Wizara imefanya mafunzo kwa Wahasibu wanaohusika kwenye usimamizi wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko huo katika ngazi ya Programu, Watekelezaji (Sub recipients) na Timu za Uendeshaji wa Mipango Kabambe ya Afya kutoka Halmashauri. Jumla ya halmashauri 98 zilipatiwa mafunzo. Aidha Wizara kupitia Mpango huo, imeweza kulipa ada za wanafunzi 1,562 wanaosoma kozi za kada za kati za afya kutoka katika vyuo vya afya hapa nchini. Sambamba na hilo Wizara imeweza kukamilisha ujenzi wa majengo mbalimbali katika vyuo vya afya vya Mvumi, Tanga na Mirembe. Vilevile, Wizara imeweza kununua magari 181 kwa ajili ya kuiwezesha MSD kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa dawa hapa nchini. Pia Wizara imeweza kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya maabara za TFDA ili

kuwawezesha kufanya kazi za uhakiki wa ubora wa dawa na chakula hapa nchini.

124. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia Kitengo cha Uimarishaji wa Mifumo ya Afya kwa kushirikiana na vitengo mbalimbali kimeweza kutekeleza shughuli mbalimbali kupitia ufadhili wa UNICEF kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uimarishaji wa mifumo ya afya ikiwemo uboreshaji huduma za mama na mtoto kwa Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe. Kitengo kimefanya Mafunzo ya kuzijengea uwezo wa kutimiza majukumu yake bodi za Afya za Halmashauri na kamati zake, Ufuatiliaji wa shughuli za huduma za Mama na Mtoto na kuzijengea uwezo na uelewa timu za usimamizi za Mikoa na Halmashauri juu ya zoezi la kupeleka fedha moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za afya (DHFF).

TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

125. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa *eHealth strategy 2013-2018*. Katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation kupitia mdau wa maendeleo PATH ilizindua Mpango wa Uwekezaji (*Digital Health Investment Recommendation Roadmap*). Mpango huu umeainisha vipaumbele vinavyohitajika vya matumizi ya mifumo ya kielektroniki ili kuboresha huduma za afya katika ngazi zote, pamoja na umuhimu wa **kukusanya taarifa na matumizi sahihi ya takwimu za sekta ya Afya kwa ujumla**. Aidha, Wizara imefungua mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za chanjo katika vituo vya Afya. Hadi kufikia Machi 2018,

jumla ya vituo **1,303** vya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro Tanga, Manyara na Dodoma vilifungiwa mfumo na kupewa vifaa vya komputa. Vilevile jumla ya watumishi **3,258** walipewa mafunzo ya jinsi ya kutumia mfumo huu.

126. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kukamilisha ufungaji wa mfumo wa kielekitroniki katika hospitali za Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa, Taasisi ya magonjwa ya saratani, Benjamin Mkapa, Mirembe, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya na Bugando. Nia ni kuhakikisha kuwa tunapunguza matumizi ya karatasi (Paperless) na kuboresha utoaji wa huduma za afya. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mdau wa maendeleo CDC/MDH inaboresha miundombinu ya ndani ya TEHAMA ijulikanayo kama Local Area Network na kuweka vifaa vya TEHAMA kama vile kompyuta katika vituo vya kutolea huduma za Afya vifuatavyo; Buguruni, Kigamboni, Tandale, Chuo Kikuu Dar es Salaam na *Infectious Disease Centre* mkoani Dar es Salaam, Vituo vya Afya Kaigara, Rwamishenye, Kayanga na Kishanje mkoani Kagera. Kazi hii itakuwa imekamilika kabla ya Juni 2018. Vilevile Wizara imekamilisha mfumo wa kupokea maoni ya wananchi juu ya ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo vya Afya nchini, ambapo mgonjwa au ndugu wa mgonjwa ataweza kutoa taarifa kupitia code namba *152*05*3#.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOPATA
RUZUKU TOKA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2017/2018**

127. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, Wizara ilitenga kiasi cha **Shilingi 785,805,952,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi, 336,300,000,000** ni fedha kutoka vyanzo vya ndani na **Shilingi 449,505,952,000** ni fedha kutoka vyanzo vya nje.

Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za Ndani.

128. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara ilipokea **shilingi 74,756,079,206.00**(Fedha za Ndani) ambazo zilitumika kutekeleza miradi ifuatayo:

- i. Ununuzi wa dawa, vifa tiba na vitendanishi
- ii. Ununuzi na usambazaji wa Chanjo za watoto chini ya miaka 5 nchini
- iii. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa Wodi ya wagonjwa wa *Private* katika Hospitali ya Taifa Muhimbili

Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za Nje.

129. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara ilipokea fedha, dawa, vifaa na vitendanishi vyenye thamani ya **shilingi 321,015,218,137.12 kutoka katika Vyanzo vya Nje** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuboresha huduma za afya nchini kwa mchanganuo ufuatao:

Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund)

Kazi zilizotekelezwa kupitia fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja zilizopokelewa na kutumiwa katika Fungu 52 ni pamoja na;

- i. kugharamia utekelezaji wa utaratibu wa malipo ya tele kwa tele kwa ajili ya Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF),
- ii. Ukusanyaji wa Damu Salama na mapitio ya Rasimu ya Sera ya Afya,
- iii. Kutoa mafunzo juu ya CCHP na PlanRep3 kwa mikoa na halmashauri,
- iv. Kufanya uhakiki wa dawa, vifaa na vifaa tiba vilivyopo nchini pamoja na kufanya uhakiki wa viashiria (Indicators) vinavyotumiwa na wadau katika kutoa fedha za Mfuko wa Pamoja (Basket Fund)
- v. Ada kwa ajili ya mafunzo ya uzamili

130. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Wizara ilipokea fedha nje ya ukomo wa bajeti **Shilingi 82,515,009,463.82** ambazo zilipelekwa moja kwa moja OR-TAMISEMI kwa ajili ya kufanya ukarabati wa Vituo vya Afya ili viweze kutoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji kwa wanawake wajawazito wanaokabiliwa na uzazi pingamizi. Kati ya fedha hizo, **shilingi 63,015,009,462.82** kutoka Benki ya Dunia na **shilingi 19,500,000,000** kutoka Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund). Fedha hizo zilitumika kugharamia utekelezaji wa miradi ifuatayo:

a) Mpango wa malipo kwa ufanisi (RBF)

Kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za afya katika **Vituo 1,325** vya Serikali vya kutolea huduma za afya katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Pwani, Tabora, Simiyu, Kigoma, Kagera na

Geita. Aidha, jumla ya **shilingi 3,425,162,919** zilipelekwa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kulipwa kama motisha kwa Timu za Uendeshaji wa shughuli za Afya za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

b) Uimarishaji wa huduma za dharura za mama na mtoto (CEmONC)

131. Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele vya Serikali katika mwaka wa fedha 2017/18 ni kupunguza vifo vya akina mama na watoto vitokanavyo na uzazi. Katika kutekeleza azma hiyo serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeanza kufanya ukarabati/ ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwemo chumba cha upasuaji, maabara, wodi ya wazazi na wodi ya watoto utakaowezesha upatikanaji wa huduma kamili za uzazi ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni, ili kupunguza vifo vya mama na watoto. Kupitia mpango huo, jumla ya vituo vya Afya 173 vinaboreshwa. Katika kutekeleza mradi huu, jumla ya **Shilingi 40,000,000,000** kutoka Banki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha Vituo vya Afya 100 na **shilingi 19,500,000,000.00** kutoka Denmark kwa ajili ya vituo vya Afya zimepelekwa katika Halmashauri mbalimbali nchini kukamilisha kazi ya ukarabati na ujenzi ambao upo katika hatua mbalimbali chini ya uangalizi wa OR-TAMISEMI na Wizara ya Afya. Aidha Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI inakamilisha mchanganuo wa vituo vya afya 21 vitakavyoboreshwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja.

Mfuko wa Dunia (Global Fund):

132. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara ilipokea fedha, dawa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye thamani ya **shilingi 303,238,541,795.37** kwa ajili ya kupambana na Kifua Kikuu, UKIMWI na Malaria.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA IDARA KUU YA AFYA

Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

133. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2017/2018, Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kutekeleza maelekezo ya Serikali kuhusu kununua dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji kwa kuingia makubaliano ya muda mrefu (Framework Agreement) na viwanda vya uzalishaji dawa. Jumla ya wazalishaji 110 tayari wana mikataba na MSD na kati ya hao wazalishaji 10 ni viwanda vya ndani. Mpango huu umewezesha MSD kufanikiwa kupunguza bei ya dawa 109 kwa wastani wa **asilimia 40**. Hali hiyo imesaidia vituo vya afya kuweza kununua dawa kwa bei nafuu na hivyo kuongeza kiasi cha dawa. Aidha, Bohari Kuu ya Dawa inaendelea kuimarisha mfumo wake wa usambazaji wa dawa ili kuhahikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma unafikia asilimia 100. Katika kufanikisha hili jumla ya magari 181 yamenunuliwa na Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo, Magari hayo yalizinduliwa na Mhe. Rais tarehe **26 Machi, 2018**. Hali hiyo imewezesha vituo vya kutolea huduma za afya kuwa na dawa muhimu kwa asilimia **89.6**. Vilevile, upatikanaji wa dawa za **ARVs** umeimarika na kuwa kati ya **asilimia 92 hadi 100**

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)

134. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuongeza wigo wa wanufaika wa bima ya afya. kufuatia utekelezaji wa mikakati hiyo, katika kipindi cha Julai 2017 hadi kufikia Machi 2018, Mfuko umeweza **kusajili idadi ya wanachama wapya wapatao 167,791** kutoka katika Sekta ya Umma na Binafsi sawa na asilimia 97 ya lengo. Hivyo idadi ya wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya imeongezeka kutoka wanachama 753,992 waliokuwa wameandikishwa mwaka 2016/17 hadi kufikia wanachama 763,068 mwezi Machi 2018. Aidha, idadi ya wanufaika nayo iliongezeka kutoka 3,491,400 mwaka 2016/17 hadi kufikia wanufaika 3,619,697 mwezi Machi 2018 sawa na asilimia 7 ya Watanzania wote. Hii inaonyesha kuwa wanachama wa Mfuko wameongezeka kwa wastani wa asilimia 10 na wanufaika asilimia 7 katika kipindi cha miaka mitano.

135. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya inaendelea na utekelezaji wa mpango wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 kaya mpya zilizoandikishwa kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) zilikuwa 66,026 na kufanya jumla ya kaya 2,096,692 zilizojiunga ukilinganisha na kaya 2,030,666 zilizokuwa zimejiunga mwaka 2016/17. Aidha, wanufaika wameongezeka kutoka 12,183,996 mwaka 2016/17 hadi kufikia wanufaika 12,580,149 Machi 2018 sawa na asilimia 25 ya Watanzania wote. Aidha, mafanikio hayo yametokana na juhudi zinazofanywa na Mfuko za kuelimisha wananchi pamoja na kubuni

mbinu mbalimbali za kuongeza wigo wa wanachama, kama kuanzishwa kwa mpango wa KIKOA (unaojumuisha kundi la wajasiriamali, vikundi vya vikoba, sacco na wavuvi), TOTO AFYA KADI (unaojumuisha watoto chini ya miaka 18), Wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya Juu, Wastaafu na wanachama binafsi.

136. *Mheshimiwa Spika*, ili kuongeza idadi ya wananchi watakao kuwa wanahudumiwa na Mfuko huu wa Serikali, Mfuko kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), unatarajia kuanzisha fao la bima linalolenga wakulima walio katika vyama vya ushirika nchini. Kupitia fao hilo lijulikanalo kama Ushirika Afya, wakulima walio katika vyama vya ushirika vya mazao ya Korosho, Pamba, Chai, Tumbaku na Kahawa watafikiwa kwa kuelimishwa na kuandikishwa kuwa wanufaika wa huduma za bima. Kufanikiwa kwa mpango kutawawezesha wakulima kupata huduma za matibabu hata kipindi ambacho si cha msimu kupitia kadi zao.

137. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imejipanga kuanza kutekeleza CHF iliyoboreshwa kuanzia mwezi Aprili, 2018. Katika maboresho hayo kila mwananchi ataweza kupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya mkoa bila kujali Kituo/Halmashauri alipojisajili tofauti na ilivyo sasa ambapo mwanachama wa CHF hupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya Halmashauri aliyojisajili tu. Kupitia Mpango huu wa CHF iliyoboreshwa, Halmashauri zitabaki na jukumu la kutoa huduma (service provider) na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) kwa kushirikiana na mfuko wa NHIF itakuwa na jukumu la kuandikisha wanufaika, kukusanya fedha za wanachama na kulipa watoa huduma (purchaser). Kiwango cha

chini cha kuchangia kwenye mfuko kitakuwa sawa kwa wananchi wote na kiinatarajiwa kuwa **Shilingi 30,0000** kwa mwaka kwa familia ya watu sita. Aidha, katika kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi, vikao vya kijiji vitapewa fursa ya kuteua maafisa watakaokuwa na jukumu la kusajili wananchama na kuwahamasisha pamoja na kukusanya michango. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa nafasi zao na ushawishi mkubwa walionao katika jamii tunayoishi, kuendelea kuwaelimisha wananchi wote umuhimu wa kujiunga na kuchangia katika mfuko huo wa bima ya afya ili waweze kupata huduma za tiba bila kikwazo cha fedha.

138. Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa CHF iliyoboreshwa ni Mkakati wa Serikali wa muda mfupi wakati tukijiandaa kuleta mswada katika bunge lako tukufu wa kuwa na Mfuko mmoja wa bima ya afya ambao kila mwananchi atalazimika kujiunga na kuchangia ili kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na uhakika wa kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pale anapohitaji. Katika Mkakati huo NHIF itapewa jukumu la kusimamia huduma za bima ya afya nchini na Mfuko wa CHF ulioboreshwa utakuwa ni sehemu ya fao moja wapo ya bima ya afya yatayokuwa yanatolewa na NHIF. Kwa msingi huo wananchi wote waliopo kwenye sekta rasmi na wale waliopo kwenye Sekta isiyo rasmi wataweza kuhudumiwa ndani ya Mfuko wa NHIF.

Mpango wa Bima kwa Wanawake Wajawazito na Watoto

139. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia NHIF na kwa kushirikiana na Benki ya Ujerumani (KfW) inatekeleza Mpango wa NHIF/CHF kwa Wanawake Wajawazito na Watoto ujulikanao kama **Tumaini la Mama.** Mpango huu ulianza kutekelezwa mwaka 2012 ambapo kina mama wajawazito hulipiwa kadi za NHIF/CHF na kuwa na uhakika wa kupata matibabu katika kipindi chote cha ujauzito na miezi sita baada ya kujifungua kwa mama na mtoto.

140. Mheshimiwa Spika, Mpango huu una lengo la kupunguza vifo vya kina mama na watoto ili kwenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya kimataifa ya maendeleo endelevu (SDGs). Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 mpaka Machi 2018, **akina mama 199,954 na watoto 20,998** walikuwa wamesajiliwa na kunufaika na mpango huu. Tangu kuanzishwa kwa mpango, tayari wanawake wapatao 875,375 wamenufaika katika mikoa ya Mbeya, Tanga, Lindi, Mtwara na Songwe.

Uboreshaji wa Huduma za Afya

141. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia NHIF ya Afya ina utaratibu wa kuvikopesha vituo vya kutolea huduma mikopo yenye lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini. Mikopo hii ni pamoja na vifaa tiba, ukarabati wa vituo, dawa na vitendanishi.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 Mfuko umetoa kiasi cha Shilingi bilioni 24 kwa ajili ya mikopo ya vifaa tiba, dawa na vitendanishi na ukarabati wa majengo kati ya Shilingi bilioni 43 zilizoidhinishwa. Kati ya hizo, Shilingi milioni 518.17 kwa ajili ya

vifaa tiba na kiasi cha Shilingi milioni 450.37 kimetolewa kwa ajili ya ukarabati wa majengo na Shilingi bilioni 23.1 kimetolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Benjamin Mkapa na ile ya Mkoa wa Dodoma. Tangu kuanzishwa kwa utaratibu huu mwaka 2009 hadi kufika Machi 2018 jumla ya Shilingi Bilioni 32 zimekwisha idhinishwa kwa vituo 375. Jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 20 kwa vituo 228 imeshatolewa. Mchanganuo zaidi umeoneshwa katika Jedwali namba 1

Jedwali 1 kuhusu Mchanganuo wa mikopo iliyotolewa kipindi cha Jan-Machi 2018

Na.	AINA YA MKOPO	KIASI	
		KILICHOIDHINISHWA	KILICHOTOLEWA
1	Ujenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa	30,000,000,000	22,764,789,759
2	Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Dodoma	3,000,000,000	363,779,600.00
3	Ununuzi wa Vifaa Tiba – vituo vya Umma	5,000,000,000	217,044,361
4	Ununuzi wa Vifaa Tiba – Sekta binafsi	3,000,000,000	301,125,500
5	Ukarabati wa Vituo vya Serikali katika Halmashauri/Mikoa mbalimbali nchini	2,000,000,000	450,373,225
	Jumla	43,000,000,000	24,097,112,445

Malipo kwa Watoa huduma

142. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Mfuko uliendelea kuwalipa watoa huduma waliosajiliwa na Mfuko ikiwa ni jukumu lake la msingi kwa huduma zitolewazo kwa wanachama wake. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, Mfuko ulilipa Watoa huduma jumla ya **Shilingi bilioni 134.92** kwa huduma mbalimbali zilizotolewa kwa wanachama sawa na asilimia 92% ya malipo ukilinganisha na kiasi cha **Shilingi 147,421.63 milioni** zilizoombwa na watoa huduma wote waliosajiliwa na kuwasilisha madai. Malipo ya madai kwa Watoa huduma hayakufanyika kwa asilimia 100 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutozingatiwa kwa miongozo ya tiba, kutozingatiwa kwa masharti ya mkataba wa huduma baina ya Mfuko na Watoa Huduma na uwasilishwaji wa madai ya udanganyifu kunakofanywa na baadhi ya watoa huduma wasio waaminifu.

143. Mheshimiwa Spika, katika kuchangia juhudi za wananchi wanaochangia CHF na kuboresha huduma zitolewazo, Serikali hutoa malipo ya tele kwa tele kwenye Halmashauri kulingana na kiwango cha makusanyo ya CHF, fedha ambazo hurejeshwa katika vituo vya kutolea huduma. Malipo yaliyofanyika kwa Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018 ni **Shilingi bilioni 1.4** na hivyo kuwezesha jumla ya **Shilingi bilioni 15.8** kulipwa kwa

Halmashauri mbalimbali nchini tangu Mfuko ulipokabidhiwa jukumu hili mwezi Julai 2009.

Mpango wa kuwapeleka Madaktari bingwa maeneo ya pembezoni

144. *Mheshimiwa Spika,* Mfuko umekuwa ukitekeleza mpango wa kupeleka Madaktari bingwa katika Mikoa ya pembezoni kila mwaka kwa huduma za kibingwa. Katika kipindi cha Julai-2017 hadi Machi 2018, mikoa 2 ya Lindi na Mtwara imeshafikiwa kwa ajili ya zoezi hili. Mikoa mingine ambayo imewahi fikiwa tangu tangu kuanzishwa kwa zoezi hili ni pamoja na; Kigoma, Rukwa, Katavi, Pwani, Shinyanga, Manyara, Mara, Simiyu, Tabora, Singida, Kagera, Ruvuma, Iringa na Njombe. Mpango huu unafanywa kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Mifupa MOI na Hospitali za Rufaa. Mpango huu umesaidia sana kufikisha huduma za matibabu za kibingwa sehemu mbalimbali hasa za pembezoni ili kuwapatia fursa wanachama na wananchi kupata huduma ambazo wangelazimika kuzifuata katika miji mikubwa zilipo hospitali hizo. Aidha, utaratibu huu umewezeshwa Madaktari wa mikoa husika kupata uzoefu na mafunzo kwa vitendo kutoka kwa madaktari bingwa. Mfuko utaendelea kutekeleza utaratibu huu kwani umekuwa wa manufaa kwa wananchi na wanufaika wa Mfuko kwa ujumla.

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (TFDA)

- 145. *Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa, inatekeleza Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano (5) wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (2017/18 - 2021/22). Utekelezaji wa kazi katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, umezingatia malengo mkakati ya taasisi ambayo ni: Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi, kuhakikisha usalama na ubora wa chakula, kuboresha huduma za maabara, kuimarisha utoaji elimu kwa umma na kuboresha huduma kwa wateja, kuimarisha uwezo wa Mamlaka katika kutoa huduma za kiudhibiti, kutoa huduma kwa waathirika wa Virusi vya UKIMWI na wenye magonjwa yasiyoambukiza, kuimarisha na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa na kuboresha masuala ya jinsia na mazingira.
- 146. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ilifanya tathmini ya maombi 1,223 (sawa na 85.1%) ya usajili wa vyakula kati ya maombi 1,437 yalipokelewa kwa ajili ya usajili wa bidhaa za chakula, ambapo maombi 1,243 yaliidhinishwa, 56 yalikataliwa kwa kutokidhi vigezo. Aidha, jumla ya sampuli 3,491 (80.7%) kati ya sampuli 4,324 za bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba zilichunguzwa, ambapo sampuli 3,163 (90.6%) zilikidhi vigezo na sampuli 328 hazikukidhi vigezo na hivyo bidhaa husika kutosajiliwa na nyingine kuondolewa kwenye soko.
- 147. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ilifanya kaguzi za viwanda 42 vya dawa katika nchi za Bangladesh, India, China, Pakistan na Misri ambapo viwanda 15 vilikidhi vigezo, 15 vilipewa maelekezo ya

kufanya marekebisho na 12 kutokidhi vigezo. Viwanda 5 vya chakula vilikaguliwa nje ya nchi katika nchi za India (2), Zambia (1), Vietnam (1) na China (1) ambapo vyote vilikidhi vigezo. Aidha, Mamlaka imeendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa makundi mbalimbali ya wananchi kuhusu madhara ya dawa, vipodozi hatarishi na usalama wa chakula pamoja na jumbe fupi zilirushwa kupitia redio, runinga, magazeti na mitandao mbalimbali ya kijamii. Vilevile, Mamlaka imeimarisha mfumo wa kieletroniki wa kupokea taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vipodozi kwa kuwezesha Watanzania kutuma taarifa kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu za mikononi kwa kupiga namba *152*00#.

148. Mheshimiwa Spika, mfumo wa kupokea taarifa za usajili wa vitendanishi kwa njia ya mtandao umetengenezwa na kuanza kutumika na hivyo kupunguwa kwa muda wa kushughulikia maombi yanayowasilishwa na wateja. Mamlaka imeweza kuweka taarifa za bidhaa zote zilizosajiliwa nchini kwenye mtandao ambao umeunganishwa na mfumo wa kielektroniki wa ndani (www.tfda.go.tz/portal/registered-products). Taarifa hizi zinasaidia wananchi na wateja kwa ujumla kuona bidhaa zilizosajiliwa na tarehe za kuisha muda wa usajili.

MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Taasisi iliyokuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilibadilishwa rasmi na kuwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa sheria Na. 8 ya mwaka 2016. Katika kuhakikisha kwamba Mamlaka inafanya kazi kwa ufanisi, mamlaka imesaini

mikataba mitatu (3) ya ununuzi wa mitambo na vifaa vya maabara vyenye thamani ya **shilingi bilioni 1.4**, vifaa hivyo vinatarajiwa kupokelewa kabla ya mwezi Juni, 2018. Aidha, ukarabati wa Maabara ya DNA Makao Makuu Dar es Salaam umeanza na unategemewa kumalizika mwezi Juni 2018. Vilevile, jumla ya sampuli **57,046** zinazojumuisha makosa ya jinai, vinasaba, maji safi, maji taka, kemikali, vyakula, dawa na bidhaa nyingine za viwandani zilipokelewa kwa ajili ya uchunguzi. Kati ya hizo ni sampuli **51,387** sawa na asilimia **88.6** ndizo zilizochunguzwa. Pia, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilifanya matengenezo kinga ya vifaa na mitambo na kununua vitendanishi ambavyo vimesaidia kutoa matokeo sahihi na kwa wakati hivyo kulinda afya na mazingira na kusaidia utoaji haki katika vyombo vya maamuzi.

150. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilitoa jumla ya **vibali 13,465** vya kemikali kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kuingiza na kusafirisha kemikali ndani na nje ya nchi. Aidha, **wadau 541** wa kemikali walisajiliwa baada ya kukidhi vigezo vinavyotakiwa katika kutoa huduma mbalimbali za kemikali hapa nchini.

TAASISI YA CHAKULA NA LISHE (TFNC)

151. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali katika kuimarisha utoaji wa huduma za Lishe nchini. Aidha, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kupunguza vifo vya watoto wadogo na wachanga nchini, Taasisi imeendelea kuratibu zoezi la kitaifa la

utoaji wa vitamini A ya nyongeza kwa watoto wenye umri kati ya miezi 6 – 59 na dawa za **kutibu minyoo** kwa watoto wenye umri wa miezi 12 – 59. Msisitizo katika kipindi hiki ulikuwa ni kufuatilia na kutoa usaidizi katika Mikoa na halmashauri ambazo zilibainika **kutofikia asilimia 90 inayopendekezwa na shirika la Afya Duniani**. Mikoa na Halmashauri hizo ni Simiyu (Bariadi), Mwanza (Magu), Shinyanga (Kishapu), Singida (Itigi), Kigoma (Buhigwe na Uvinza), Katavi (Mpanda), Rukwa (Nkasi) na Tabora (Uyui). Vilevile, katika kipindi hiki, Taasisi ilikamilisha maandalizi ya mpango kazi wa kuzuia upungufu wa madini joto mwilini; mpango unaoainisha kazi mbalimbali zinazolenga kuimarisha upatikanaji na matumizi ya chumvi yenye madini joto katika jamii.

152. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Chakula na Lishe kwa kushirikiana na Taasisi ya *Food and Nutrition Institute iliyopo Zurich – Switzerland* ilifanya utafiti wa kubaini Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa kwa Kiashiria cha Madini-joto kwa Wanawake Walio Kwenye Umri wa Kuzaa. Utafiti huu ulifanyika katika Kata ya Kilema (Kati na Juu) katika Wilaya ya Moshi Vijijini ambapo ulihusisha Sampuli 211 zilizochukuliwa kwa awamu mbili za hali ya hewa tofauti; awamu ya kwanza mwezi Julai (kipindi cha baridi) na awamu ya pili mwezi Oktoba (kipindi cha joto). Vilevile, Taasisi inatarajia kufanya tafiti zenye lengo la kupata majibu ya kisayansi kuhusu njia bora, inayokubalika na endelevu ya kuwasaidia wasichana walioko shuleni na nyumbani kupata virutubishi vya nyongeza (micronutrient supplements) ili kuwakinga na tatizo la upungufu wa damu mwilini.

153. Mheshimiwa Spika, Katika kufuatilia kiwango cha ufanisi katika utekelezaji wa afua za lishe nchini na kuhimiza uwajibikaji kwa watoa huduma, Wizara imeanza kutumia Kadi Alama ya Lishe (Nutrition Score Card). Kadi Alama hii ina jumla ya viashiria **18** ambavyo vinatumika kufuatilia utekelezaji wa afua za lishe na matumizi ya kadi hii yamezingatia uzoefu uliopatikana katika matumizi ya kadi alama nyingine zilizopo nchini kama ile ya Malaria na ile ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto. Kutokana na ufanisi mkubwa katika matumizi ya kadi alama hii, Serikali ya Ethiopia ilituma wataalam wake sita kutoka Wizara ya Afya kuja Tanzania kujifunza jinsi ya kuandaa na kutumia mfumo huu kuwezesha kadi alama ya lishe ili ianze kutumika katika nchi hiyo.

154. Mheshimiwa Spika Taasisi kwa kushirikiana na OR- TAMISEMI iliandaa mikutano mahsusi ya kuwahamasisha viongozi na watendaji wa Mikoa na Halmashauri kuhusu kubaini na kujumuisha afua za lishe katika mipango na bajeti za Mikoa na Halmashauri husika. Mikutano hiyo iliwashirikisha washiriki wapatao 700 ambao ni Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa, Wakuu wa Idara (Afya, Mipango, Kilimo na Mifungo) na Makatibu wa Afya ngazi ya Halmashauri, Maafisa Lishe na Wadau wa Llishe kutoka baadhi ya Asasi zisizo za Kiserikali (NGOs). Zoezi hili lilihusisha pia uhamasishaji kuhusu Mpango Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (NMNAP), pamoja na kuhamasisha Halmashauri kutenga kiasi cha **Shilingi 1,000** kwa kila mtoto chini ya miaka mitano kwa ajili ya utekelezaji wa afua za kupambana na udumavu.

155. Mheshimiwa Spika, Taasisi inaendelea kutoa msaada wa kitaaluma kwa kuendesha mafunzo kuhusu matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto waliolazwa hospitalini (in-patient management of acute malnutrition) katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kipindi hiki, watoa huduma **274** wamenufaika na mafunzo hayo katika Mikoa ya Lindi, Shinyanga, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Dodoma, Simiyu na Ruvuma. Aidha, Taasisi imeendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya katika vituo vya tiba vinavyotoa huduma kuhusu lishe na matunzo kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Mafunzo haya yalifanyika katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tanga, Mtwara, Lindi na Arusha, ambapo Watoa huduma wapatao **622** na watu **15,832** wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye utapiamlo walinufaika kupitia mafunzo haya ambapo wagonjwa walipatiwa pia matibabu kwa kutumia chakula dawa (Ready to Use Therapeutic Foods) na kupatiwa ushauri nasaha wa lishe bora.

TAASISI YA UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU (NIMR)

156. *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu kupitia Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa ya Binadamu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya Utafiti. Taasisi imefanya tafiti mbalimbali ikiwemo tafiti za Majaribio ya Chanjo ya UKIMWI, Tiba Mbadala, Afya ya mama na mtoto, Malaria na TB. Matokeo ya tafiti hizi yamesaidia kuandaa afua mbalimbali za kuboresha huduma kwa waathirika wa magonjwa hayo. Aidha, tafiti kwenye afya ya mama na mtoto zinalenga kuboresha mfumo wa afya hasa upatikanaji wa huduma ikiwemo chanjo, elimu ya lische na hatua za kupunguza vifo vya mama na watoto chini ya miaka 5. Taasisi kwa kushirikiana na Wizara na wadau wa Afya imefanya tathmini ya uwepo wa maji salama na usafi wa mazingira (WASH) katika vituo vya afya mbalimbali vinavyotoa huduma za kujifungua. Taarifa zilizopatikana kutokana na utafiti huo ni kwamba, pamoja na Serikali kupitia Sekta ya Afya kuisitiza wananchi kwenda kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za Afya, bado yapo mapungufu makubwa ikiwa ni pamoja na yafuatayo; Asilimia 19 ya vituo hutumia maji toka vyanzo visivyoboreshwa vikiwemo vyanzo wazi kama mito na mabwawa na visima visivyoboreshwa; Asilimia 46.5 ya sampuli za maji zilizopimwa zilionekana kuwa na vimelea vya maambukizi ya magonjwa mbalimbali; Asilimia 42 ya vyumba vya kuzalia havikuwa na sehemu za kunawia mikono; Asilimia 10 ya vituo hasa zahanati vilikuwa na vyoo duni visivyoboreshwa na kuleta hatari ya maambukizi.

157. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imejipanga kufanyia kazi matokeo yaliyobainishwa na utafiti huo kwa kuelekeza msukumo mkubwa katika eneo la afya Kinga ikiwa ni pamoja na kushirikiana na OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kuondoa changamoto zilizobainishwa na utafiti huo.

158. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia NIMR imeendelea kufanya tafiti za dawa asili zinazoonisha matumaini ya awali katika kupunguza makali au kutibu magonjwa ya malaria, UKIMWI na magonjwa nyemelezi, ugonjwa wa Ini, shinikizo la damu, kisukari na kupunguza lehemu mwilini, uvimbe wa **tezi dume kwa wanaume na dawa inayoongeza nguvu za kiume** kwa wanaume. Baadhi ya dawa hizo zinatayarishwa kwa ajili ya usajili na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania.

BARAZA LA FAMASIA

159. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa karibu na wananchi waishio vijijini, Wizara kupitia Baraza la Famasia imesajili jumla ya maduka ya Dawa Muhimu **1,255** yaliyopo katika Mkoa ya Tanga, Mara, Morogoro, Mbeya, Geita, Pwani, Mwanza, Mtwara, Lindi, Arusha, Simiyu, Kagera, Ruvuma, Dodoma, Njombe na Singida. Hadi sasa kuna maduka ya Dawa Muhimu kufikia **11,763** yaliyosajiliwa ambalo ni ongezeko la asilimia **10.6** ikilinganishwa na maduka **10,508** ya mwaka 2016.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU CHINI YA IDARA KUU MAENDELEO YA JAMII

Uwezeshaji Wanawake

160. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imeendelea kuratibu utendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuzihimiza Halmashauri kuchangia asilimia 5 ya mapato yao ya ndani katika Mfuko. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2017, **Halmashauri 130** kati ya **185** zilichangia **Shilingi bilioni 7.3** katika Mfuko ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 8.9** zilizochangiwa na Halmashauri kwa mwaka 2016/17. Fedha zilizochangiwa ni sawa na **asilimia 26** ya **Shilingi bilioni 28.3** zilizopaswa kuchangiwa kwa mwaka 2017/18. Fedha hizo zilitolewa kama mikopo kwa **vikundi 4,365** vyenye **wanawake wajasiriamali 39,449** . Natarajia kuwa, hadi kufikia mwezi Juni, 2018, uchangiaji wa mapato ya ndani kwa kila Halmashauri utaongezeka. Hivyo, natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuhakikisha wanachangia fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kama wanavyopaswa.

161. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mtwara imeviwezesha **vikundi vinne vyenye wanawake wajasiriamali 20** kupata stadi za ujasiriamali na uendeshaji biashara, utunzaji wa kumbukumbu, uwekaji akiba na marejesho baada ya kupatiwa mikopo yenye thamani ya **Shilingi milioni 69** kutoka fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake zilizotolewa moja kwa moja na Wizara. Aidha, kutokana na stadi na mikopo hiyo wanawake hao wamewezeshwa kuchimba mabwawa mawili na

kuyajengea uzio kwa ajili ya ufugaji wa samaki, kupanua eneo la kilimo cha mbogamboga kutoka ekari nne hadi kufikia ekari nane na kupanua ujenzi wa mabanda kwa ajili ya ufugaji wa kuku.

162. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI iliratibu uhamasishaji wa wanawake kuanzisha na kujiunga na vikundi vya kiuchumi (SACCOS na VICOBA) kwa kufanya majaribio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Uhamasishaji wa Wanawake Kuanzisha na Kujiunga na Vikundi vya Kiuchumi katika Halmashauri za Rombo mkoani Kilimanjaro na Mvomero mkoani Morogoro. Kutokana na uhamasishaji huo, **jumla ya vikundi 88** vyenye **wanachama 1,807 (Ke 1,517 na Me 290)** vilianzishwa vikiwemo VICOBA na Vikundi vya Hisa. Vikundi hivyo vimewawezesha wanachama kuchangia na kukuza mitaji yenye thamani ya Shilingi milioni 50 ambayo imewawezesha kuanzisha na kuwekeza katika biashara na miradi mbalimbali ya uzalishaji ikiwemo kilimo na ufugaji.

163. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imezindua na kuratibu utekelezaji wa **Programu ya Kikundi Mlezi**. Programu hii inalenga kuwalea wajasiriamali wanawake wanaoanza kwa kuwaunganisha na wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na vikundi vya kiuchumi vinavyofanya vizuri ili waweze kujifunza mbinu na stadi za ujasiriamali. Programu inatekelezwa katika mikoa 6 ya Pwani, Kigoma, Songwe, Katavi, Rukwa na Mbeya. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2018, jumla ya **wanawake wajasiriamali 30** waliunganishwa na **vikundi 25** vinavyofanya vizuri vilivyopo katika mikoa hiyo. Aidha, katika

Programu ya Kikundi Mlezi, **wanawake 1,131** waliwezesha kupata mafunzo ya urasimishaji na uboreshaji wa bidhaa wanazozalisha kwa kuwaunganisha na mamlaka za udhibiti na usimamizi ikiwemo Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali za uendeshaji wa biashara na miradi yao.

164. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo SIDO, Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) na Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi iliendelea kuwezesha ushiriki wa wanawake katika Maonesho ya Biashara ya Kitaifa na Kimataifa. Katika mwaka 2017/18, **wanawake wajasiriamali 1,183** kutoka mikoa **26** ya Tanzania Bara waliwezesha kushiriki katika Maonesho ya Sabasaba, Juakali, Nanenane na VICOBA. Kutokana na ushiriki huo, wanawake wajasiriamali waliweza kujifunza mbinu mbalimbali za kuboresha bidhaa na kupata uzoefu kuhusu upatikanaji wa masoko kutoka kwa washiriki wa mikoa mingine na nchi nyingine.

165. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) imeendelea kutoa huduma za fedha ikiwa ni pamoja na mikopo yenye riba nafuu na mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali hususan wanawake katika mikoa **saba ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Iringa, Ruvuma, Njombe na Mbeya**. Katika mwaka 2017/18, **wajasiriamali 6,237 (Ke 5,097 na Me 1,140)** walipatiwa mikopo ikilinganishwa na **wajasiriamali 6,267 (Ke 4,596 na Me 1,671)** mwaka 2016/17. Juhudi hizi

zimewesha **wajasiriamali 87,063 (Ke 71,744 na Me 15,319)** kupata mikopo tangu mwaka 2010. Kwa upande wa thamani ya mikopo iliyotolewa mwaka 2017/18, benki ilitoa mikopo ya **Shilingi bilioni 10.1** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 13.3** mwaka 2016. Thamani ya mikopo iliyotolewa tangu mwaka 2010 mpaka Machi, 2018 ni **Shilingi bilioni 131.9**.

166. Mheshimiwa Spika, Aidha, Benki ya Wanawake Tanzania imefungua **vituo 244** vya kutolea mikopo na mafunzo kwa wanawake wajasiriamali katika mikoa ya Dar es Salaam (115), Mwanza (46), Dodoma (27), Mbeya (5), Iringa (9), Ruvuma (24) na Njombe (18) katika mwaka 2017/18 ikilinganishwa **na vituo 88** mwaka 2016/17 sawa na ongezeko **la asilimia 177**. Benki ya Wanawake Tanzania pia iliwapatia wananchi uelewa kuhusu kujiwekea akiba akiba kwa kile wanachokipata kwa kufungua akaunti. Katika mwaka 2017/18, jumla ya **akaunti 10,415 (Ke 7,811 na Me 2,604)** zilifunguliwa hadi kufikia **akaunti 88,397** Machi, 2018 katika matawi mawili ya Benki ya Wanawake Tanzania (**tawi la Mkwepu na Mjasiriamali**) kutoka mwaka 2009. Kati ya akaunti hizo, **akaunti 65,419 ni za wateja wanawake sawa na asilimia 74, akaunti 20,961 za wanaume na akaunti 2,017 za makampuni**

167. Mheshimiwa Spika, ukatili wa kijinsia bado ni tatizo hapa nchini. Takwimu za Jeshi la Polisi kwa mwaka 2017, zinaonyesha kuwa, matukio ya ukatili wa kijinsia yalikuwa 41,416 mwaka 2017 ikilinganishwa na matukio 31,996 mwaka 2016. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara yangu imekuwa ikiratibu utekelezaji wa

Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22). Lengo la mpango huu ni kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imezijengea uwezo Kamati za Ulinzi na Usalama wa Wanawake na Watoto za ngazi ya mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uratibu na namna ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia hususan dhidi ya wanawake na watoto. Jumla ya waratibu 52 toka katika ngazi ya Mkoa wamejengewe uwezo wa kuratibu afua za kukabiliana na ukatili. Vile vile Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 za: Kasulu (W), Kasulu (TC), Kibondo, Kakonko, Kibaha, Ludewa, Kaliua, Wanging'ombe, Rungwe, Kyela, Mbeya (DC), Kiteto, Mkuranga, Busega, Busenga, Dodoma (M), Uyui, Tabora (M) na Rufiji

Maendeleo ya Jamiii

168. Mheshimiwa Spika, Wizara, inaendelea **kuamsha ari ya Wananchi kushiriki katika kujiletea maendeleo yao sambamba na kushiriki shughuli za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo** kwa kutumia nguvu kazi pamoja na rasilimali zinazowazunguka katika maeneo yao. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Wizara imefanya uhamasishaji katika Mikoa 11 ya Iringa, Dodoma, Mwanza, Pwani, Kigoma, Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Kagera na Shinyanga. Uhamasishaji huu umewezesha ujenzi wa majengo ya Kituo cha Afya Mondo, Wilaya ya Misungwi (Mwanza); ujenzi wa bwawa la maji Maghangu Mpwapwa (Dodoma); ujenzi wa Zahanati Ufyambe (Iringa); ujenzi wa shule ya sekondari na kituo cha afya – Uvinza (Kigoma); ujenzi wa shule ya sekondari na kituo cha afya – Mpanda (Katavi); ujenzi wa kituo

cha afya – Sumbawanga (Rukwa); ujenzi wa kituo cha afya – Mbozi (Songwe); ujenzi wa shule ya sekondari – Manispaa ya Mbeya (Mbeya); kuchangia fedha na vifaa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa Makazi ya wazee (Kagera); kuzindua Kituo cha Mkono kwa Mkono (One Stop Centre) cha wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili wa watoto Wilaya ya Kahama (Shinyanga) na ujenzi wa madarasa mawili katika Kijiji cha Chambasi, Kisarawe (Pwani). Miradi hii iligharimu kiasi cha Shilingi 229,127,100, kati ya hizo mchango wa wananchi ni Shilingi 112,341,250 sawa na asilimia 49.03. Fedha hii imesaidia Serikali kuokoa gharama na kuijengea jamii umiliki endelevu wa miradi mbalimbali wanayoianzisha katika maeneo yao.

169. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18 **wataalamu wa maendeleo ya jamii 175** kutoka Sekretarieti za Mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 walijengewa uwezo wa kuamsha ari ya wananchi kushiriki kwenye uchumi wa viwanda, utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 - 2021/22) na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi hususani katika kuzalisha mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ambayo ni malighafi ya viwanda vidogo vidogo na vya kati katika maeneo yao.

170. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu **uzalishaji wa wataalam wa Maendeleo ya Jamii** kutoka katika vyuo 8 vya maendeleo ya jamii vya Buhare, Mlale, Misungwi, Rungemba, Mabughai, Ruaha, Uyole na Monduli. Vyuo hivyo hutoa mafunzo ya Maendeleo ya jamii katika ngazi ya Cheti na

Stashahada. Katika mwaka 2017/18, jumla ya **wanafunzi 1,588** (Ke 984 na Me 604) **walidahiliwa** ikilinganishwa na 3,248 (Ke 1,987 na Me 1,261) mwaka 2016/17. Aidha, katika mwaka 2017/18, jumla ya **wanafunzi 3,320** (Ke 1,947 na Me 1,373) **walihitimu** katika Vyuu 8 vya Maendeleo ya Jamii ikilinganishwa na **wahitimu 3,694** (Ke 2,228 na Me 1,466) mwaka, 2016/17.

171. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imefanya mapitio ya mtaala wa mafunzo ya Vyuu vya Maendeleo ya jamii ili kupata wahitimu mahiri wenye kuendana na mahitaji ya soko la ajira kwa sasa pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Mtaala huo utatumika katika Vyuu 6 vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Ruaha, Uyole, Mlale, Monduli na Rungemba. Kwa upande wa vyuo vya maendeleo ya jamii-Ufundi mitaala yao ilifanyiwa mapitio mwaka 2016/17.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

172. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuweka mazingira wezeshi ya kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2018, jumla ya **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 192 yalisajiliwa**. Kati ya mashirika yaliyosajiliwa, **mashirika 21** yalisajiliwa katika ngazi ya Kimataifa, **162** katika ngazi ya Kitaifa na **Mashirika 9** ngazi ya Wilaya. Usajili huu umewezesha jumla ya **mashirika 8,211** kusajiliwa nchini kuanzia mwaka 2005 hadi Machi, 2018 (**Kiambatanisho Na.5**). Mashirika haya yamechangia uboreshaji wa huduma za kijamii katika nyanja za afya, elimu, maji, mazingira, kilimo, haki za binadamu, utawala bora, jinsia, ufugaji na uvuvi, wanyama pori na nishati.

173. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mashirika haya yanaendesha shughuli zao kwa matakwa ya sheria na taratibu za nchi, **Wizara ilihakiki mashirika** na hadi kufikia Machi, 2018, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **4,868** yalikuwa yamehakikiwa. Aidha, katika uhakiki huo, wizara imebaini jumla ya **mashirika 513** yenye sifa za mashirika ambayo yaliyokuwa yamesajiliwa chini ya Sheria nyingine na kuyajumuisha chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24 ya mwaka 2002. Hatua hii imesaidia kuimarisha uratibu na usimamizi mzuri wa mashirika haya katika misingi ya uwazi, utoaji taarifa na uwajibikaji kwa jamii.

Haki na Maendeleo ya Mtoto

174. Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya watoto bado ni tatizo kubwa hapa nchini. Kwa mujibu wa Takwimu za Jeshi la Polisi Kuhusu Hali ya Uhalifu kwa mwaka 2017, **matukio ya ukatili dhidi ya watoto yalikuwa 13,457** ikilinganishwa na **matukio 10,551** mwaka 2016 sawa na ongezeko la **asilimia 28**. Ongezeko hili tunaamini ni kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na Serikali pamoja na wadau wa maendeleo ya mtoto kuhusu malezi katika familia na jamii kuelewa umuhimu wa kutoa taarifa za matukio katika Mamlaka husika. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22). Katika mwaka 2017/18, Kazi zilizofanyika chini ya mpango huu ni **kutoa elimu kuhusu athari za mila na desturi zenye madhara kwa jamii ikiwemo ukeketaji, mimba na ndoa za utotoni** kwa makundi mbalimbali katika jamii.

Jumla ya **wananchi 13,020** walipatiwa elimu wakiwemo wanafunzi 8,546, walimu 476, wazee wa mila 56, viongozi wa dini 64, ngariba 38, waendesha bodaboda 168, wazazi/walezi 3,600 na watendaji 72 kutoka mikoa ya Shinyanga, Mara, Tabora, Lindi, Dodoma, Tanga, Dar es Salaam na Katavi.

175. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuwapatia huduma watoto waliofanyiwa ukatili kupitia **Huduma ya Simu kwa Watoto (Child Help Line)**. Katika mwaka 2017/18, simu 18,464 zilipokelewa kuhusu ukatili dhidi ya watoto. Kati ya simu hizo, simu za watoto 1,072 (Ke 621 na Me 451) ziliwezesha kupata huduma (chakula, vifaa vya shule na huduma za sheria na afya) ikilinganishwa na simu za watoto **441 (Ke 325 na Me 96)** waliopata huduma mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia **143**.

176. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuchukua hatua ili **kuzuia ukatili dhidi ya watoto** kwa kuwajengea uwezo **watoa huduma kwa wahanga wa ukatili 1,192** kuhusu namna ya kushughulikia mashauri ya watoto ili kuboresha huduma hizo. Watoa huduma hao ni pamoja na: Maafisa Upelelezi wa mikoa ya Kipolisi, Maafisa Polisi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii na wajumbe wa Timu za Ulinzi na Usalama wa Mtoto kutoka Halmashauri **15 katika mikoa 7**.

177. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya watoto wa kike yamekuwa yakikutana na vikwazo mbalimbali ikiwemo **mimba na ndoa za utotoni**. Kwa mujibu wa Tafiti ya Afya ya Uzazi na Mtoto na

Viashiria vya Malaria Tanzania ya mwaka 2015-16, mimba za utotoni ni asilimia 27. Mikoa inayoongoza ni Katavi (45%), Tabora (43%), Dodoma (39%), Morogoro (39%) na Mara (37%). Katika kukabiliana na ndoa na mimba za utotoni, Wizara imezindua **Kampeni ya Kuzuia Mimba za Utotoni ya "Mimi Msichana Najitambua: Elimu ndiyo Mpango Mzima"** Uzinduzi huo ulifanyika katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, Tarime - Mara tarehe 11/10/2017. Kampeni hii imelenga kutoa hamasa kwa watoto wa kike kutumia klabu katika shule za msingi na sekondari ili kuelekeza muda wao mwingi katika elimu, kujitambua na kutoa taarifa za ukiukaji wa haki zao. Aidha, wananchi 13,284 wakiwemo, wanafunzi (8,546), walimu (476), Viongozi wa dini (110), wazee wa mila na watu mashuhuri (90), ngariba (38), waendesha bodaboda (261), wazazi/walezi (3,600) na watendaji wa vijiji (113) kutoka mikoa ya Shinyanga, Tabora, Lindi, Dodoma, Dar es Salaam, Tanga, Mara na Katavi walipewa elimu kuhusu madhara ya mimba na ndoa za utotoni.

178. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha **watoto wanashiriki katika maendeleo yao** na kujitambua, kwa mwaka 2017/18 Wizara imeendelea kuwezesha ushiriki wa watoto katika mabaraza na klabu za wasichana za Kujikinga na mimba za utotoni. Jumla ya **mabaraza ya watoto 13 na klabu 600** katika shule za msingi na sekondari zimeanzishwa kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 na kufikia idadi ya **mabaraza 1,669 na Klabu 2,000.**

Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto

179. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto walio chini ya miaka mitano walio katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (Day Care Centres) vya Serikali na Binafsi. Kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, **vituo 139** vilipatiwa **usajili** ikilinganishwa na vituo **270** vilivyopatiwa usajili mwaka 2016/17 na hivyo kufikia **vituo 1,046** vilivyosajiliwa nchi nzima. Aidha, watoto 6,075 (Ke 4,018 na Me 2,057) waliandikishwa katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana 2016/17 ikilinganishwa na watoto 4,450 (Ke 3,097, Me 1,353) mwaka 2015/16.

180. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Walezi wa Watoto wanakuwa na uwezo wa kutoa **malezi stahiki katika vituo vya kulelea watoto wadogo** mchana (Day Care Centres). Katika kufanikisha azma hii, Walezi 600 kutoka Manispaa ya Temeke, Ubungo, Kigamboni na Ilala walijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo kuhusu programu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ikiwemo uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza vituo kuajiri walezi wenye sifa. Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya Walezi wa Watoto 1,882 walikuwepo katika vituo ikilinganishwa na **Walezi 1,652** mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la **asilimia 14**.

181. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea **kuzalisha wataalamu wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto** katika Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara. Jumla ya wanafunzi 83 (Ke 58 na Me 25) walidahiliwa kwa mwaka

2017/18 ikilinganishwa na wanafunzi 56 (Ke 39 na Me 17) waliodahiliwa mwaka 2016/17. Aidha, wanafunzi 52 (Ke 35 na Me 17) wahitimu katika mwaka 2017/18 ikilinganishwa na wahitimu 8 wote wanawake mwaka 2016/17.

Huduma za Ustawi kwa Watoto

182. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na Asasi Zisizo za Kiserikali imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma za msingi za malezi, matunzo na ulinzi kwa **watoto walio katika mazingira hatarishi nchini.** Jumla ya **watoto 6,132 (Ke 2,972 na Me 3,160)** walio katika mazingira hatarishi walipatiwa huduma za msingi katika **makao ya watoto 157** yanayoendeshwa na Taasisi za dini, Mashirika ya watu binafsi na Serikali (**Kiambatanisho Na. 6**) ikilinganishwa na **watoto 4,515 (Ke 2519 na Me 1,996)** mwaka 2016/17. Kati ya watoto hao, **watoto 78 (Ke 43 na Me 35)** wanaishi katika Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini ambayo yanamilikiwa na Serikali. Aidha, Kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla **ya leseni 14 za usajili wa Makao ya watoto** zimetolewa ikilinganishwa na leseni 50 kwa mwaka 2016/17 na kufikia idadi ya makao 157 nchi nzima. Kati ya makao hayo, **moja ni la Serikali na 156** yanamilikiwa na kuendeshwa na watu binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya kijamii au Taasisi za kidini. **Nitumie fursa hii kuwataka watu/Taasisi zote zinazotoa huduma za malezi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu kujisajili katika Halmashauri zao mara moja.**

183. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Railway Children Afrika (RCA) imefanya zoezi la utambuzi wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani katika Halmashauri za Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Ubungo, Arusha, Iringa, Mbeya Jiji, Wilaya ya Mbeya, Dodoma, Nyamagana na Ilemela. Jumla ya **watoto 6,393 (Ke 1,528 na Me 4,865)** walitambuliwa wakiishi na kufanya kazi mtaani katika kipindi cha Disemba, 2017 hadi Januari, 2018. Kati yao, **watoto 1,385 (Ke 410 na Me 975)** walitambuliwa wakiishi na kufanya kazi mtaani kwa muda wa usiku. Wizara inatekeleza mkakati wa kushughulikia tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani kwa kuwaunganisha watoto na familia zao. Kati ya watoto waliotambuliwa, **watoto 952 (Ke 83 na Me 869)** wameunganishwa na familia zao.

184. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa **watoto walio katika mkinzano na Sheria** wanapata haki za msingi ikiwa ni pamoja na huduma za sheria na elimu katika mahabusu tano za watoto za Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Katika mwaka 2017/18, jumla ya **watoto 291 (Ke 13 na Me 278)** walio katika mkinzano na sheria waliwezesha kupata huduma za msingi (chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu na elimu) ikiwa ni pamoja na huduma za msaada wa kisheria ikilinganishwa na watoto **255 (Ke 18 na Me 237)** mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la **asilimia 14**. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam imeboresha miundombinu katika mahabusu ya watoto Dar es Salaam kwa kuchimba kisima cha maji sambamba na usimikaji wa tenki la maji lenye ujazo wa lita 10,000.

185. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria imewachepusha **watoto 126 (Ke 24 na Me 102)** kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao ikilinganishwa na **watoto 72 (Ke 8 na Me 64)** waliochepushwa mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la **asilimia 67**. Aidha, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuwezesha huduma za msingi (chakula, malazi, mavazi na huduma za matibabu) ikiwa ni pamoja na marekebisho ya tabia, elimu na mafunzo kwa **watoto wa kiume 35** waliobainika na makosa ya jinai waliopo katika **Shule ya Maadilisho Irambo Mbeya** ikilinganishwa na **watoto 72** mwaka 2016/17. Katika kipindi hiki Shule ya Maadilisho ilishika nafasi ya kwanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwenye mtihani wa Moko wa Taifa wa Darasa la Saba na watoto wote walifaulu mtihani wa Darasa la Saba.

186. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI imeendelea na juhudi ya kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika ngazi ya familia kulingana na Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009 kwa kutoa **huduma za malezi ya kambo na uasili**. Wizara imewezesha **watoto 44 (Ke 24 na Me 20)** kuwekwa chini ya malezi ya kambo ikilinganishwa na **watoto 54 (Ke 21 na Me 33)** mwaka 2016/17. Aidha, **watoto 17 (Me 8 na Ke 9) waliasiliwa** mwaka 2017/18 ikilinganishwa na **watoto 21 (Ke 11 na Me 10)** mwaka 2016/17.

187. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwatambua Watu wa Kuaminika (Fit Persons) ili kulea watoto walio katika mazingira

hatarishi. Juhudi hii imewezesha **Watu wa Kuaminika 187** kutambuliwa katika Halmashauri 19 mwaka 2017/18. Hadi kufikia Machi, 2018, jumla ya **watoto 243** wamepitia kwenye familia za watu wa kuaminika katika Halmashauri 19 za Magu DC, Kasulu DC, Kasulu TC, Musoma Dc, Iringa MC, Iringa DC, Mufindi DC, Njombe DC, Makete DC, Mbeya Jiji, Mbeya DC, Mbarali DC, Hai DC, Temeke DC, Arusha DC, Kakonko DC, Kibondo DC, Misenyi DC na Chunya DC. Watu wa kuaminika huchaguliwa na wanajamii ili kulea watoto walio katika mazingira hatarishi.

Huduma za Ustawi kwa Wazee

188. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa **huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza**. Katika mwaka 2017/18, jumla ya wazee wasiojiweza 517 (Ke 250 na Me 267) wanaoishi katika **makazi 17 ya Serikali** walipatiwa huduma za msingi - chakula, malazi, mavazi na matibabu (**Kimbatanisho Na.7**) ikilinganishwa na wazee 465 (Ke 221 na Me 244) mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia 11. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha mazingira ya kutolea huduma za ustawi wa jamii katika makazi 17 ya wazee ya Serikali kwa kujenga bweni la kukaa **wazee 20 (Ke 10 na Me 10)** katika Makazi ya Wazee Kolandoto na uwezesaji wa vifaa ikiwa ni pamoja na bajaji 10, vifaa vya jikoni na vifaa vya huduma ya kwanza katika Makazi 17 ya Wazee ya Serikali.

189. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana OR - TAMISEMI iliwezesha **wazee 506,943 (Ke 220,312 na Me 286,631)**

kupata vitambulisho vya matibabu bure katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2018 ikilinganishwa na wazee 74,590 waliopata vitambulisho vya matibabu bure mwaka 2016/17. Juhudi hizi zimewezesha kufikia idadi ya **wazee 581,533 (Ke 254,793 na Me 326,740)** waliopata vitambulisho ikiwa ni **asilimia 35** ya **wazee 1,657,206** waliotambuliwa katika Halmashauri zote **(Kiambatanisho Na. 8)**. Kupatiwa vitambulisho hivi ni hatua ya mpito kuelekea kuwapatia wazee walengwa Bima za afya ili waweze kupata matibabu bora bila vikwazo. Aidha, katika Maadhimisho ya **Siku ya Wazee Duniani** yaliyofanyika tarehe 01/10/2017 mjini Dodoma, Wizara iliwezesha **wazee 320** kupima afya zao na kupatiwa ushauri wa kitabibu.

Huduma za Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa na mashauri ya matunzo kwa watoto

190. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa lililopo chini ya usimamizi wa Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Ofisi za Ustawi wa Jamii za Halmashauri zimeendelea kutoa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa kwa familia. Kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya **mashauri ya migogoro ya ndoa 13,382** yalipokelewa na kufanyiwa usuluhishi katika Halmashauri mbalimbali nchini na Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii **(Kiambatanisho Na.9)** ikilinganishwa na **mashauri ya migogoro ya ndoa 8,454** mwaka 2016/17. Kati ya mashauri hayo, mashauri **11,326 sawa na asilimia 85 yamesuluhishwa** na yamekamilika, mashauri 1,397 sawa na asilimia 10 yamepelekwa mahakamani na mashauri 659 sawa na asilimia 5 yanaendelea na usuluhishi.

191. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa, watoto wanapata matunzo kutoka kwa wazazi, Wizara imeendelea kufanyia kazi mashauri ya matunzo ya watoto nchini. Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya **mashauri ya matunzo ya watoto 11,815** yalipokelewa. Kati ya mashauri hayo, 4,965 yalihusu matunzo ya watoto walio ndani ya migogoro ya ndoa na 5,708 watoto waliozaliwa nje ya ndoa Kati ya **mashauri yaliyopokelewa, 10,673** yalikamilika kuwezesha huduma kwa watoto na mashauri 1,142 yaliyopewa rufaa kwenda mahakamani ikilinganishwa mashauri ya matunzo ya watoto 12,406 yaliyokamilika mwaka 2016/17 (matunzo ya watoto walio kwenye migogoro ya ndoa 6,557, matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa 4,133 na mashauri 1,716 yaliyopewa rufaa kwenda mahakamani).

USHIRIKIANO WA NDANI NA NJE YA NCHI

192. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wadau wa sekta itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za maendeleo na ustawi wa jamii kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuhamasisha na kufikisha ujumbe kwa umma. Baadhi ya siku hizo ni Siku ya Wanawake, Watoto, Familia, Wazee na Mtoto wa Kike.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI

YA IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII

Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru

193. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru **ilidahili jumla ya wanafunzi 1,169** katika fani ya Maendeleo ya Jamii ikiwa ni ongezeko la **asilimia 86** ya udahili wa **wanafunzi 628** mwaka 2016/17. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, **wanafunzi 486** walidahiliwa katika ngazi ya cheti, **wanafunzi 83 Stashahada** na **wanafunzi 600 ngazi ya Shahada**. Aidha, **wanafunzi 684 waliohitimu** mwaka 2017/18 ikilinganishwa na **wahitimu 609** mwaka 2016/17 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 12**.

194. Mheshimiwa Spika, Taasisi pia **imefanya tafiti** tatu ambazo ni Tathmini ya mahitaji ya Ushiriki wa Jamii katika kijiji cha Kikwe wilaya ya Arumeru, tafiti kuhusu watoto walio katika mazingira hatarishi katika sekta isiyo rasmi katika Wilaya ya Arumeru (utafiti kuhusu watoto katika masoko ya jamii) na Tathmini ya changamoto inayowakabili Maafisa Maendeleo ya Jamii Tanzania katika Halmashauri. Matokeo ya tafiti hizi yatawezesha Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Wizara kuboresha utoaji wa mafunzo na utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya jamii.

Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama

195. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Kijitonyama imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti, Diploma, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2017/18, Taasisi **ilidahili wanafunzi 1,185 (Ke 811 na Me 374)** katika fani zitolewazo katika ngazi mbalimbali ikiwa

upungufu wa **asilimia 6.91 ya wanafunzi 1,273** waliodahiliwa mwaka 2016/17. Upungufu huu umetokana na kuzuiliwa kudahili wanafunzi katika kozi za jioni kwa ngazi ya Shahada. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, wanafunzi 421 walidahiliwa katika ngazi za Cheti, 409 Diploma, 315 Shahada, 28 Stashahada ya Uzamili na 12 Shahada ya Uzamili. Aidha, **wanafunzi 1,122 (Ke 722 na Me 400) walihitimu** mwaka 2016/17 katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,172 (Ke 789, Me 383) waliohitimu mwaka 2015/16 sawa na **ongezeko la asilimia 4.2.**

196. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama imeendelea kuboresha majengo na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kufanya ukarabati wa jengo lenye **madarasa 8 na ujenzi wa maktaba awamu ya 6 umekamilika na awamu ya 7** imeanza. Aidha, Taasisi imewezesha **watumishi wanne** kuhudhuria mafunzo katika fani na ngazi mbalimbali za masomo. Kati yao, wawili waliwezesha kuhudhuria masomo katika ngazi ya **Uzamili na wawili ngazi ya Uzamivu.**

C: VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2018/19

197. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kupitia fungu 52 (Idara kuu ya Afya) imejiwekea vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini;

- i) Kuimarisha huduma za chanjo kwa watoto ili kuendelea kubaki katika viwango vya juu vya utoaji wa huduma za chanjo ili kuwaepusha watoto na magonjwa yanayoweze kuepukika kwa chanjo
- ii) Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayotokana na kutozingatia kanuni za usafi na usafi wa mazingira kama magonjwa ya kuhara, kuhara damu na kipindupindu kwa kuongeza uhamasishaji na usimamizi wa usafi na usafi wa mazingira.
- iii) Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kama magonjwa ya moyo, kisukari na saratani kwa kuhamasisha jamii kuepukana na tabia hatarishi na kujijengea tabia ya kufanya mazoezi mara kwa mara na kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa ili kujiepusha na hatari ya kupata magonjwa hayo.
- iv) Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto nchini ili kupunguza idadi ya vifo vya wanawake na watoto vinavyotokana na Uzazi kwa kukarabati na kujenga Wodi Maalum kwa ajili ya Watoto wachanga (Neonatal Care Units) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 7 na Wodi za Wazazi na kujenga vyumba vya wagonjwa mahututi (ICU) wanaotokana na uzazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

(5) mitano yenye viwango vikubwa vya vifo vitokanavyo na uzazi.

- v) Kupunguza maambukizi ya Malaria, TB na VVU/UKIMWI;
- vi) Kuimarisha upatikanaji wa damu salama nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Vituo 12) kukusanyia Damu Salama (*Satellite Blood Banks*) katika mikoa 12 yenye uhitaji.
- vii) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za za afya nckiahini
- viii) Kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa nchini katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maaluma na za Kitaifa ili kusogeza huduma hizi karibu zaidi na wananchi na kupunguza rufaa za nje ya nchi zisizo na ulazima
- ix) Kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo vya afya vinavyomilikiwa na Serikali
- x) Kuboresha vyuo vya mafunzo ya afya ili kuendelea kuzalisha wataalam wenye ubora kwa kufanya upanuzi na ujenzi wa majengo na ukarabati kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Afya vya Uuguzi vya Nachingwea, Kibondo, Kagemu, Kondo, Same na Kiomboi; Vyuo vya Mafunzo ya Maafisa Afya vya Bombo Tanga, Mpwapwa na Ngudu Mwanza; vyuo vya Maafisa Tabibu vya Kibaha, Tanga na katika Chuo cha Maabara cha Singida
- xi) Kuimarisha Mifumo ya Habari, Takwimu na Teknolojia ili kurahisisha upatikanaji wa Takwimu katika sekta ya Afya.

- xii) Kuimarisha mfumo wa ugharimiaji wa huduma za afya nchini kwa kuongeza wigo wa huduma za bima ya afya kwa wananchi ili kufikia malengo ya kuwa na bima kwa wananchi wote na kufikia lengo la afya kwa wote (Universal Health Coverage – UHC).

198. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2018/19, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

HUDUMA ZA KINGA

199. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2018/19, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za huduma za kinga ikiwa ni pamoja na;

- i. Kununua na kusambaza **chanjo za watoto** kulingana na mahitaji ya nchi ambapo jumla ya **shilingi bilioni 30** zimetengwa.
- ii. Kuendelea kutoa chanjo ya kwa wasichana wenye miaka kati ya 9 – 14 ili kukabiliana na saratani ya mlango wa kizazi nchi nzima
- iii. Kuongeza wigo na kasi ya uibuaji na tiba kwa wagonjwa wa kifua kikuu katika mikoa yote nchini, ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 5** kimetengwa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa vifaa (catridges) na dawa kwa ajili ya **uchunguzi na matibabu ya kifua kikuu.**

Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

- i. Kukarabati na kujenga Wodi Maalum kwa ajili ya Watoto wachanga (Neonatal Care Units) katika Hospitali za Rufaa za

Mikoa 7 ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Rukwa, Kilimanjaro, Iringa na Kigoma ambapo **shilingi milioni 900** zimetengwa.

- ii. Kupanua Wodi za Wazazi na kutenga vyumba vya wagonjwa mahututi wanaotokana na uzazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa (5) ya Mbeya, Shinyanga, Morogoro, Pwani na Kigoma mitano ya ambapo, **shilingi bilioni 1** zimetengwa.
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya damu salama kwa kujenga **Vituo 12** vya kukusanyia Damu Salama (Satellite Blood Banks) katika mikoa 12 ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 4.3** kimetengwa
- iv. Kununua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango katika vituo vya kutolea huduma nchini ambapo Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 22.5**
- v. Kununua dawa za malaria kwa ajili ya kinamama wajawazito (Sulphadoxine +pyrimethamine), dawa za kuokoa maisha ya mama wajawazito ikiwa ni pamoja na oxytocin (dawa ya kuzuia kutokwa) na damu baada ya kujifungua, magnesium sulphate (kwa ajili ya kifafa cha mimba), Fefol (kwa ajili ya kuongeza damu) pamoja na Viuadudu (Biolarvicides) ambapo **shilingi bilioni 8.5** zimetengwa.
- vi. Kununua na kusambaza vitanda, magodoro, mashuka na vitanda vya kuzalia mama wajawazito ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 4.9** kimetengwa
- vii. Kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni kwa

kusimamia ukamilishaji wa ukarabati vituo vya afya 208 ili viweze kutoa huduma ya upasuaji kwa akina mama wanaokabiliwa na uzazi pingamizi

- viii. Kutoa chanjo ya kwa wasichana wenye miaka kati ya 9 - 14 ili kukabiliana na saratani ya mlango wa kizazi nchini

HUDUMA ZA TIBA

Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi.

200. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2018/19 Wizara itaendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi nchini kwa kununua na kuvisambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya. **Jumla ya shilingi bilioni 270 zimetengwa.** Aidha, ili Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma kwa kununua vitanda, magodoro, mashuka na kuvigawa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima ambapo **shilingi bilioni 4.9** zimetengwa

Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya kibingwa

201. Mheshimiwa Spika katika mwaka 2018/19, **Wizara itaendelea** kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za matibabu ya kibingwa nchini ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuendelea na huduma za kupandikiza figo (renal transplant) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Benjami Mkapa
- ii. Kuendelea kutoa huduma za upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia kwa kuweka *cochlear implants* katika Hospitali ya Taifa Muhimbili
- iii. Kuendelea na ujenzi wa jengo maalum kwa wagonjwa wanaolipia (private wing) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ambapo jumla ya **shilingi bilioni 16** zimetengwa.

- iv. Kuanzisha Mfuko wa kugharamia Vipandikizi (*Establish revolving fund for procurement of implants*) katika Taasisi ya Mifupa (MOI) ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 4.2** kimetengwa
- v. Kununua na kusimika vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ya Saratani katika Taasisi ya Saratani Ocean Road ikiwa ni pamoja na PET Scan **ambapo kiasi cha shilingi bilioni 14.5 zimetengwa.**
- vi. Kuendelea na ujenzi wa jengo na kusimikia vifaa vya uchunguzi (X-Ray Building), pamoja na kununua vifaa vya tiba ya mionzi, katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 5** zimetengwa.
- vii. Wizara itaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara ili kusogeza huduma za afya za kibingwa kwa wananchi wa kanda hiyo, ambapo, kiasi cha **shilingi bilioni 1** kimetengwa.
- viii. Wizara imepanga kununua *Ambulances 27* kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa rufaa Nchini

Ukarabati na ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa

202. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara imetenga kiasi cha **shilingi bilioni 30** kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kutekeleza kazi zifuatazo;

- i) Ukarabati wa Miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

- ii) Kuanzisha na kuboresha vitengo vya dharura (Emergency Units) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa
- iii) Ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa katika Mikoa ya Katavi, Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Mara

Uhakiki wa Ubora wa Huduma za Afya

203. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ubora wa huduma za afya nchini, Wizara imekamilisha Mwongozo wa Viwango vya Msingi kwa Vituo vya kutolea huduma za afya nchini (Basic Health Facilities Standards) ambao utanza kutumika mwaka 2018/19. Aidha, Wizara itafanya tathmini ya Ubora wa Huduma zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini vya umma na kuvipatia hadhi stahiki pamoja na kuvisajili na kuvipatia leseni kulingana na mwongozo huo.

204. Mheshimiwa Spika, Wizara iko katika hatua za mwisho za majadiliano na Global Fund ili kupata fedha za kufanya maboresho ya huduma katika hospitali za rufaa za mkoa 9, hospitali ngazi ya halmashauri 25, vituo vya afya 21 na zahanati 156 baada ya kufanyiwa tathmini na kupewa nyota. Vituo hivi viko katika mikoa ya Kilimanjaro, Mara, Rukwa, Tanga, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Njombe na Songwe. Kiasi cha fedha zitakazotumiwa ni **milioni 20** kwa kila zahanati, **milioni 50** kwa kila kituo cha afya, **milioni 100** kwa kila hospitali ya halmashauri, na **milioni 200** kwa kila hospitali ya mkoa.

Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya

205. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia eneo la rasilimali watu katika ya afya kwa kufanya ukarabati na upanuzi wa vyuo afya ambapo jumla ya **shilingi bilioni 8** zimetengwa

**VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2018/19 - FUNGU
53**

206. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kupitia Fungu 53 itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

- (i) Kukuza usawa wa jinsia na uwezesaji wa wanawake kiuchumi;
- (ii) Kuimarisha upatikanaji wa haki na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto;
- (iii) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22 ili kupunguza ukatili dhidi yao kwa asilimia 50;
- (iv) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama;
- (v) Kuboresha majengo na miundombinu katika makazi ya wazee, Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini, mahabusu za watoto na Shule ya Maadilisho
- (vi) Kuweka mazingira wezeshi ili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa; na
- (vii) Kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo.

207. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2018/19, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

Kukuza Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake

208. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kwa:

- (i) Kuratibu uhamasishaji wanawake wa kuanzisha na kujiunga na vikundi vya kiuchumi ikiwemo SACCOS na VICOBA na kuwaunganisha wanawake na fursa za mikopo;
- (ii) Kuwezesha uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mipango na Mikakati ya Sekta; na
- (iii) Kuendelea kutokomeza ukatili wa kijinsia hususan dhidi ya wanawake kwa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22.

Maendeleo Jamii

209. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kutekeleza yafuatayo:

- (i) Kuendelea kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika miradi ya maendeleo katika maeneo yao;
- (ii) Kufanya tathmini ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996; na
- (iii) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

210. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo na ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) Kuendelea kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;
- (ii) Kuendelea kufuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha yanatoa mchango unaotarajiwa kwa maendeleo na kufuata Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24 ya mwaka 2002; na
- (iii) Kutathmini utendaji wa Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001.

Haki na Maendeleo ya Mtoto

211. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha 2018/19, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha watoto wanapata haki zao kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) Kutathmini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008;
- (ii) Kuimarisha hali ya upatikanaji wa haki za msingi za mtoto;
- (iii) Kukuza ari na mwamko wa jamii katika kulinda haki na ustawi wa maendeleo yam toto; na
- (iv) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 –

2021/22.

Huduma za Ustawi wa Jamii

212. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutekeleza na kuboresha yafuatayo;

- (i) Kuwezesha upatikanaji wa huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto;
- (ii) Kutoa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na watoto walio katika mkinzano na sheria;
- (iii) Kusajili makao ya watoto walio katika mazingira hatarishi;
- (iv) Kuimarisha hali ya upatikanaji wa haki na huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza; na
- (v) Kutoa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa katika familia.

Rasilimali Watu katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii

213. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya maendeleo na ustawi wa jamii katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii, Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama. Katika mwaka 2018/19 shughuli zifuatazo zitatekelezwa:

- (i) Kudahili **wanafunzi watarajiwa 6,848.** Kati yao,

wanafunzi 3,653 katika Vyuho nane vya Maendeleo ya Jamii, **wanafunzi 50** Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara, **wanafunzi 1,200** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na **wanafunzi 1,945** Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama;

- (ii) Kuendelea kugharamia mafunzo ya uzamili na uzamivu kwa Wakufunzi na Wahadhiri wa kada mbalimbali;
- (iii) Kuendelea kuboresha miundombinu katika Vyuho vya Maendeleo ya Jamii (Mlale na Misungwi); na
- (iv) Kuendelea kuajiri Wakufunzi na Wahadhiri katika Vyuho vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara.

D: SHUKRANI

214. *Mheshimiwa Spika*, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark (DANIDA), Uswisi (SDC), Korea Kusini (KOICA), Ireland (Irish Aid), Canada (DFATD) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia na UNICEF kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Pia, napenda kuzishukuru nchi za Canada, China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa njia mbalimbali.

215. *Mheshimiwa Spika*, vilevile nayashukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), GAVI, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo (UNDP), UNFPA, UN-Women, Shirika la Afya Duniani (WHO) na Benki ya Dunia (WB). Wengine ni Abbott Fund, BASIC NEED (UK), ACF – Canada, Baylor College of Medicine ya Marekani, Canadian Bar Association, CDC, CORDAID (Netherlands), CUAMM, DANIDA, DFID, Engender Health (USA), EED, Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF), Family Health International (FHI360), FINIDA, GIZ, Good Samaritan Foundation (GSF), German TB and Leprosy Relief Association (GLRA), HelpAge International, ILO, Jane Adams School of Social

Work ya Chuo Kikuu cha Illinois Marekani, John Snow Incorporation (JSI), KfW, Global Partnership for Education (GPE), Madaktari Afrika na Madaktari Wasio na Mipaka (Medicins Sans Frontieres – MSF), MSERIOR, ORIO, P4H, SAREC, SDC, SIDA (Sweden), Shirika la Upasuaji la Spain, SIGN la Marekani, na Shirika la Human Resource Capacity Project, Touch Foundation, USAID na, Children Investment Foundation Fund (CIFF), World Lung Foundation.

216. *Mheshimiwa Spika*, tunawashukuru pia Wadau wa Maendeleo ambao ni African Programme for Orchorceriasis Control, Africare, Axios International, Aids Relief Consortium, AIHA, ASCP, ASM, APHL, Balm and Gillead Foundation, Bill and Melinda Gates Foundation, Clinton Health Access Initiative, CLSI, CMB, Christoffel Blinden Mission (CBM), Christian Relief Services (CRS), Department of Defence ya Marekani, Community of Saint Egidio (DREAM), Duke University, ECSA, Futures Group, Glaxo Smith Kline (GSK), General Electric (GE – USA), Havard University na University of Maryland, Helen Keller International, Henry Jackson Foundation, IMA, ICAP, International Trachoma Initiative, Intrahealth, International Eye Foundation, I-TECH, Jhpiego, Johns Hopkins University, Labiofarm Industry, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Management Science for Health (MSH), MEDA, Merck & Company, Malaria No More, Military Advancement for Medical Research, NOVARTIS, Pathfinder, PATH, President’s Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR), Pharm Access International, PactWorld, Plan International, Pfizer, Qiagen, Research Triangle Institute (RTI), Regional Psychosocial Support Initiatives (REPSSI), Saint Thomas Hospital- London, Save the Children, SightSavers International, Global Health Supply Chain (GHSC) na University of Columbia, URC,

USA-Presidential Malaria Initiative (PMI), World Vision, FXB, Walter REED Army Institute of Research (WRAIR) na World Education Inc.

217. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, naomba kuwashukuru **Dkt. Mpoki M. Ulisubisya** Katibu Mkuu (Afya) na **Bibi Sihaba Nkinga** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Muhammad Bakari Kambi**, Mganga Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia, Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Prof. Lawrence Museru, Mkurugenzi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) Dr. Respicious Boniface Rwezimula; Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janabi; Mkurugenzi wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI); Dr. Julius Mwaiselage; na Mkurugenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) Dkt. Alphonse Chandika; Mkurugenzi wa Hospitali Maalum ya Kibong'oto Dkt. Riziki Kisonga, Mkurugenzi wa Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe Dkt. Erasmus Mndeme, Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya Dkt. Godlove Mbwaji; Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando Dkt Abel Makubi; Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya KCMC Dkt Gilead Masenga. Aidha, nichukue fursa hii pia kuzishukuru Taasisi zilizo chini ya

Wizara pamoja na Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini (FBOs), ya kujitolea na Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa waendeleo kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu.

218. *Mheshimiwa Spika*, natumia fursa hii kuishukuru familia yangu, kwa upendo na uvumilivu na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha Napenda kuwashukuru wananchi wote wa Mkoa wa Tanga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuendeleza Mkoa wetu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa akili na nguvu zangu zote ili kuleta Maendeleo katika Mkoa wetu.

**E: MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA
KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

Fungu 52 - Afya

Mapato

- 219. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya **Shilingi 240,042,508,157.00** Kati ya fedha hizo **Shilingi 220,267,010,057.00** zitakusanywa katika mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara na **Shilingi 19,775,498,100.00** ni kutoka makao makuu.

Matumizi ya Kawaida

- 220. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 304,473,476,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 88,465,756,000.00** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 216,007,720,000.00** zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

Miradi ya Maendeleo

- 221. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 561,759,999,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 184,959,999,000** na fedha za nje ni **Shilingi 376,800,000,000.00**

**Jumla ya Makadirio ya Bajeti kwa 2018/19 kwa Fungu 52 ni
Shilingi 866,233,475,000.00**

Fungu 53 – Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Mapato

222. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara imekadiria kukusanya **Shilingi 3,090,796,000** kutokana na ada za wanafunzi kutoka Vyuu 8 vya Maendeleo ya Jamii na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara, ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mauzo ya vitabu vya zabuni.

Matumizi Kwa mwaka 2018/19

223. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/19 inakadiriwa kuwa **Shilingi 32,140,649,000**. Kati ya makadirio hayo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 27,226,804,000** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 4,913,845,000**.

Matumizi ya Kawaida

224. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 27,226,804,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,116,962,000** ni Mishahara ya watumishi na **Shilingi 12,109,842,000** ni Matumizi Mengineyo.

Miradi ya Maendeleo

225. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 4,913,845,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,500,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,413,845,000** ni fedha za nje.

- 226. Mheshimiwa Spika,** Jumla kuu ya fedha inayoombwa kwa mwaka 2018/19, kwa Fungu 53 ni **Shilingi 32,140,649,000.**
- 227. Mheshimiwa Spika,** Jumla kuu ya fedha inayoombwa kwa mwaka 2018/19, **Shilingi 898,374,124,000**
- 228. Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto www.moh.go.tz. na www.mcdgc.go.tz.
- 229. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.